# Nipashe

Jumanne Agosti 25, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580319

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Upatikanaji vitambulisho vya NIDA bado ni tatizo

UKURASA 3


Nipashe TESA
Jumanne Agosti 25, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Maisha bora yalivyojikita kilimohai, viuatilifu asilia
Usafiri wa anga kurudi mbwa anaponusa virusi vya corona
ELIMU
NA BEATRICE PHILEMON
Ni habari mbaya mamia wanavyokwama kusoma

UKURASA 11

# Panga la mwisho

**VIGEZO** vitakavyotumiwa na NEC leo kuamua wagombea urais, ubunge na udiwani hadharani ...*Endelea uk. 2*




## Butiku avipa neno vyombo vya dola uchaguzi Oktoba

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## WARIOBA AOMBA MAGUFULI ASAIDIWE

UKURASA 3

MICHEZO YANGA YAMALIZA NA CARLINHOS, YACOUBA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Panga la mwisho

**Na Waandishi Wetu**

MCHAKATO wa uteuzi wa wagombea urais, ubunge na udiwani katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, unakamilika rasmi leo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) itakapoanika orodha ya waliokidhi vigezo na kuteuliwa.

Kwa mujibu wa ratiba ya NEC, fomu za kuomba kuteuliwa kwa nafasi ya rais zilianza kutolewa Agosti 5 hadi 25 mwaka huu huku zile za nafasi ya ubunge na udiwani zikianza kutolewa Agosti 12 hadi 25, mwaka huu.

Mwenyekiti wa NEC, Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, alisema jana jijini Dodoma kuwa uteuzi wa wagombea wa kiti cha rais na makamu wa rais utafanyika ofisi za tume jijini huku wa ubunge ukifanyika ofisi za wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo husika na kwa udiwani uteuzi utafanyika ofisi za wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata.

Alisema fomu za uteuzi zitawekwa eneo la wazi hadi saa 10 jioni Agosti 26, mwaka huu na wagombea watapata nafasi ya kuweka pingamizi.

Mwenyekiti huyo alisema wengine wanaoruhusiwa kuweka pingamizi ni Mkurugenzi wa Uchaguzi, Wasimamizi wa Uchaguzi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Msajili wa Vyama vya siasa.

Aliwaagiza wasimamizi wa uchaguzi kuwapo kwenye ofisi zao leo wakati wote kuanzia saa moja asubuhi hadi saa 10 jioni, na kitendo cha kutokuwapo ofisini katika muda huo, tume itachukua hatua kali dhidi yao.

"Tume inarudia kuvikumbusha vyama vya siasa kuzingatia maelekezo yaliyomo katika maadili ya uchaguzi hasa katika eneo la kuzitumia kamati za maadili kutatua migogoro na malalamiko yatakayojitokeza," alisema.

Alipoulizwa kuhusu malalamiko ya wagombea wa upinzani kunyimwa fomu, kiongozi huyo wa tume alisema wana taarifa na wamechukua hatua zinazopaswa.

Kwa mujibu wa Mkurugezi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, vyama vya siasa 17 kati ya 19 venye usajili wa kudumu, vimechukua fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Miongoni mwa vyama hivyo ni Chama cha Mapinduzi (CCM kinachowakilishwa na Rais John Magufuli, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kilichomteua Tundu Lissu na AAFP kilichomsimamisha Seif Maalim Seif.

Wengine waliochukua fomu na vyama vyao kwenye mabano ni Philipo Fumbo (DP), Leopold, Mahona (NRA), Muttamwega Mgaywa (SAU), Queen Sendiga (ADC), Twalib Kadege (UPDP), Bernard Membe (ACT Wazalendo).

Cecilia Mmanga (Demokrasia Makini), Hashim Spunda(CHAUMMA), Khalfani Mazrui (UMD), David Mwaijolele (CCK), Profesa Ibrahim Lipumba (CUF), Yeremia Maganja (NCCR Mageuzi), John Shibuda (ADA-TADEA) na Maisha Muchunguzi(NLD).

**VIGEZO 10 URAIS**

Akitoa maelezo ya vigezo kwa wagombea urais wakati wakichukua fomu hivi karibuni, Dk. Mahera alisema kwa mujibu wa kifungu cha 37(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, fomu hizo sharti ziwasilishwe siyo zaidi ya saa 10:00 jioni siku ya uteuzi.

Dk. Mahera pia alisema kwa mujibu wa Kanuni ya 37(1) na (2) vya kanuni za uchaguzi wa rais na wabunge za mwaka 2020, wagombea wa nafasi ya kiti cha rais na makamu wa rais watatakiwa kujaza fomu namba 8A na fomu namba 10 za maadili ya uchaguzi ili kutimiza masharti ya kuteuliwa.

Pia, alisema kifungu cha 30 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, kimeweka utaratibu unaopaswa kufuatwa ili mtu ateuliwe kuwa mgombea wa kiti cha rais na makamu wa rais kwamba awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, awe ametimiza umri wa miaka arobaini (40), awe mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa.

Vilevile, awe anazo sifa za kumwezesha kuwa mbunge au mjumbe wa baraza la wawakilishi na asiwe ametiwa hatiani na mahakama yoyote kwa kosa la kukwepa kulipa kodi yoyote ya serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi.

Pamoja na sifa hizo, mgombea wa kiti cha rais au makamu wa rais ni lazima awe amedhaminiwa na watu wasiopungua 200 waliojiandikisha kupiga kura katika kila mkoa kwa mikoa 10 na kati ya hiyo angalau mikoa miwili iwe ya Tanzania Zanzibar.

Vigezo hivyo pia vinamtaka mtiania awe ameweka dhamana ya Sh. milioni moja Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Dhamana hiyo itarejeshwa kwa mgombea baada ya uchaguzi endapo atakuwa amepata sehemu moja ya kumi (1/10) au zaidi ya kura zote halali zilizopigwa na awe amekula kiapo mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani kwamba anazo sifa zinazotakiwa, hajapoteza sifa hizo na kwamba anakubali kuwa mgombea. Pia, wagombea kwa nafasi hizo wanatakiwa kuwa na wadhamini ambao wamejiandikisha kuwa wapigakura kwenye mikoa wanayoishi, hawajamdhamini mgombea mwingine yeyote wa kiti cha urais au umakamu wa rais.

Kigezo hicho kinafafanuliwa zaidi kuwa wadhamini hao siyo lazima wawe wanachama wa chama kilichompendekeza wala siyo lazima wawe wanachama wa chama chochote cha siasa na wawe wamewadhamini wagombea kwa kutumia fomu ya uteuzi.

**VIGEZO UBUNGE**

Kwa mujibu wa Ibara ya 67(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mtu yeyote atakuwa na sifa za kustahili kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa mbunge endapo ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ametimiza umri wa miaka 21.

Sifa nyingine ni kujua kusoma na kuandika kwa Kiswahili au Kiingereza, ni mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa na hajawahi kutiwa hatiani na mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi.

Sharti lingine ni awe amedhaminiwa na wapigakura wasiopungua 25 walioandikishwa kuwa wapigakura katika jimbo husika.

Mgombea kwa nafasi hiyo pia anatakiwa awe ametoa tamko mbele ya hakimu kuthibitisha kwamba anazo sifa zinazotakiwa kugombea ubunge na hajapoteza sifa hizo.

Pia, anatakiwa aweke dhamana ya Sh. 50,000 kwa msimamizi wa uchaguzi kupitia akaunti ya amana ya halmashauri atakayopatiwa siku atakayochukua fomu za uteuzi.

Vilevile, taratibu za uteuzi zinamtaka mgombea wa ubunge kujaza fomu namba 8B inayohusu taarifa zake binafsi na zithibitishwe na chama kilichomteua ngazi ya mkoa, wilaya au jimbo kwamba ni za kweli.

Pia anatakiwa kujaza fomu namba 10 ya tamko la kuheshimu na kutekeleza maadili ya uchaguzi na anatakiwa awasilishe nakala nne za fomu ya uteuzi kwa msimamizi wa uchaguzi siyo zaidi ya saa 10:00 jioni siku ya uteuzi.

**VIGEZO UDIWANI**

Kwa upande wa wagombea wa udiwani, kifungu cha 39 2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, kinaainisha sifa za mgombea udiwani kuwa ni pamoja na kuwa raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 21, anayejua kusoma na kuandika kwa Kiswahili au Kiingereza, awe mkazi wa kawaida wa halmashauri anayogombea, awe mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa chenye usajili wa kudumu.

Mgombea huyo pia awe na kipato halali kinachomwezesha kuishi na awe hajatiwa hatiani na mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi.

Mgombea udiwani pia anapaswa atimize masharti kadhaa ikiwa ni pamoja na kudhaminiwa na wapigakura wasiopungua 10 walioandikishwa katika kata anayogombea, awe ametoa tamko mbele ya hakimu kuthibitisha kwamba anazo sifa za kugombea udiwani na hajapoteza sifa hizo.

Pia, anatakiwa awe ameweka dhamana ya Sh. 5,000 kwa msimamizi wa uchaguzi kupitia akaunti ya amana ya halmashauri atakayopatiwa siku ya kuchukua fomu za uteuzi.

Ratiba ya NEC inaonyesha kuwa uchaguzi huo kampeni za uchaguzi katika nafasi zote zitaanza 26 Agosti, yaani kesho hadi 27 Oktoba na uchaguzi wenyewe utafanyika Jumatano Oktoba 28, mwaka huu.

*Imeandikwa na Augusta Njoji (DODOMA) na Thobias Mwanakatwe (DAR)

# Butiku avipa neno vyombo vya dola uchaguzi Oktoba

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, amevitaka vyombo vya dola nchini kutoonea yeyote kwenye uchaguzi mkuu badala yake vitende haki na kuwapa wananchi nafasi ya kufanya uamuzi wa kuchagua viongozi wao.

Akizungumza jana kwenye kongamano la maombi na dua kuhusu uchaguzi mkuu jijini Dodoma, lililoandaliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), alisema uchaguzi unatoa nafasi mara moja kwa wananchi wenye nchi yao kufanya uamuzi wa nani awe kiongozi wao na kwamba waachwe wapige kura bara na visiwani kwa uhuru.

"Nyote mnaoshiriki kuwezesha mchakato wa uchaguzi msiwaonee wananchi wa Tanzania wasinyang'anywe uhuru, nafasi yao na msitende vituko katika kuwapa nafasi ya kupiga kura, uwe polisi, jeshi au usalama wa taifa au uwe nani, wapeni uhuru wapige kura kwa uhuru na kwa heshima," alisema.

"Mambo haya tulikuwa tunatenda siku za nyuma yaishe kuanzia kikao hiki (cha viongozi wa dini), watu wa dini mtusaidie mtuombee wale wote wanayoyafanya Mungu awatazame, siwezi kusema awatazame kwa jicho gani, lakini Mungu anajua," alisisitiza.

"Kwanini mnakwenda kuwaomba kura, hata maaskofu tunawachagua siku hizi kwa sababu nchi ni yetu, wananchi nchi ni yao, nchi si yako unayekwenda kugombea, unakwenda kuomba ridhaa yao uwaongoze, uende kwa heshima na adabu, alisema.

Butiku alisema: "Uende kwa wananchi kwa adabu, usiende unatembeza fedha unataka kuwahonga, unatumia umaskini wao kutaka kuwahonga, mtu wa namna hiyo nadhani ni Ibilisi, mnakwenda kudhalilisha wananchi unaotakiwa kuwaeleza utafanya nini wakikuchagua."

Alivitaka vyama vya siasa nchini kuacha kupinga uongozi uliopo madarakani.

Alisema pamoja na kuwa vyama vya siasa vinatakiwa kupinga serikali iliyoko madarakani kutokana na sera zao, lakini havipaswi kutumia matusi katika kufikisha ujumbe wao.

"Kwanza nivipongeze vyama vya siasa kwa kazi vinazofanya kwani bado ni vichanga vimeanzishwa mwaka 1992, lakini lazima viendelee kujifunza namna sahihi ya kupinga na siyo kutukana matusi Rais," alisema Butiku.

Alisema kitendo cha vyama vya upinzani kumtukana rais, huo sio uafrika bali ni mambo ya kuiga mataifa mengine ya ambayo yamekuwa na matukio kama hayo.

Akizungumzia uchaguzi mkuu 2020, Butiku alisema wagombe wote wanatakiwa kwenda kwa wananchi kwa heshima na siyo kutumia fedha zao kutoa rushwa ili wachaguliwe.

Katibu Mkuu wa Kamati ya Taifa ya Maridhiano, Askofu Oswald Mlay, alisema lengo la kongamano hilo, ni kuliombea taifa kuelekea uchaguzi mkuu mwa huu, ili upite kwa amani na haki.

Alisema pamoja na kuombea uchaguzi mkuu, pia wanampongeza Rais Magufuli kwa jitihada za kuleta maendeleo alizozifanya katika kipindi cha miaka mitano ya muhula wa kwanza wa uongozi wake.

"Rais wetu amefanya mambo makubwa sana katika taifa letu, wakati wa mikutano ya kampeni mwaka 2015 alisema hata kwenda Ulaya na amefanya kweli... amekuwa Rais wa kwanza Afrika kumaliza miaka mitano ya utawala wake bila kwenda," alisema.

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, akizungumza katika kongamano hilo, aliyataka makanisa na misikiti nchini kuacha kujihusisha na siasa katika kipindi hichi cha kuelekea uchaguzi mkuu 2020.

## HABARI KITAIFA

# Upatikanaji vitambulisho vya NIDA bado ni tatizo

**Na Mary Geofrey**

WAKATI kampuni za mawasiliano ya simu nchini zikiwataka wateja wake kusajili laini zao kwa mfumo wa alama za vidole, baadhi ya wananchi wameendelea kulalamikia ugumu wa upatikanaji wa vitambulisho vya kitaifa.

Jana, kampuni za mawasiliano ya simu za Airtel, Halotel, Smile, Tigo, Vodacom na Zantel, zilitoa taarifa kwa umma kupitia magazeti, zikiwahimiza wateja wake kusajili laini zao kwa mfumo huo mpya.

Taarifa hiyo iliwataka watumiaji wa simu hizo kujisajili kwa alama za vidole ili kuendelea kupata huduma za mawasiliano nchini na kuepuka udanganyifu.

Hata hivyo, baadhi ya wakazi wa Ilala jijini Dar es Salaam waliozungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki iliyopita, walidai kusubiri kwa muda mrefu kupatiwa vitambulisho hivyo bila mafanikio.

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kupitia kwa Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Hifadhi Hati, Geofrey Tengeneza, ilisema inaendelea kutoa huduma kwenye maeneo yote nchini.

Tengeneza alisema NIDA ofisi zao ziko wazi wakati wote na waliendelea kutoa huduma kwa wananchi hata wakati wa baa la corona.

"Kuna taasisi hazitoi huduma kwa namba nyingine isipokuwa za NIDA, hivyo tulishirikiana nao kuwapa mwongozo wa kutumia namba za vitambulisho kwa wale waliojiandikisha kwa njia ya mtandao ili kutoa huduma kwa jamii," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa Aprili Mosi mwaka huu na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, Watanzania milioni sita waliokuwa wamepata vitambulisho vya taifa kati ya Watanzania milioni 27 waliostahili kupata vitambulisho hivyo.

Alisema serikali imeshanunua mashine mpya yenye thamani ya Sh. bilioni 8.5 yenye uwezo wa kufyatua vitambulisho 9,000 kwa saa ambayo ingetakiwa kuanza kufanya kazi Aprili mwaka huu.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma wa Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA), Semu Mwakyanjala, akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, alisema jumla ya laini za simu zilizosajiliwa kwa mfumo wa alama za vidole hadi kufika Juni 30 mwaka huu ni milioni 43.848.

Alibainisha kuwa laini ambazo hazijasajiliwa kwa mfumo wa alama za vidole hadi kufikia Juni 30 mwaka huu ni milioni 4.283.

"Jumla ya Watanzania wanaotumia simu za mkononi ni milioni 48.132 na waliosajiliwa kwa alama za vidole ni asilimia 91.1," alisema na kuongeza kuwa kuanzia Januari 21 hadi Juni 30 mwaka huu, laini ya simu za mkononi zilizofungwa kwa kutosajiliwa kwa alama za vidole ni milioni 9.07.

Mwakyanjala alisema jumla ya laini zilizosajiliwa upya baada ya kufungiwa ni milioni 2.76 na kwamba laini milioni 26 nchini zinatumia huduma ya intaneti na milioni 26 zinatumia huduma za kibenki.

# Warioba aomba Magufuli asaidiwe

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, amesema Rais John Magufuli anahitaji msaada mkubwa katika mapambano dhidi ya rushwa kwa sababu kwa sasa inatolewa na viongozi.

Akifungua kongamano la Maadhimisho ya Kumbukizi ya Mwalimu Nyerere, Jaji Warioba alisema, Rais Magufuli amekuja na ajenda inayosema nchi irudishe nidhamu, uadilifu, kupambana na ufisadi na rushwa ili kulinda rasilimali.

"Ajenda hii ni muhimu kwa nchi yetu hata mimi ninaunga mkono ajenda hii, sheria, kanuni zinatungwa watu wameshughulikiwa, lakini kazi bado inahitaji msaada.

"Siku hizi viongozi wanahonga na kuhongwa kila sehemu kwenye serikali hasa katika uchaguzi vyama vya siasa hata kwenye michezo, taasisi binafsi na kwa wanafunzi kuna rushwa na hali ni mbaya," alisema.

Alisema wakati wa uchaguzi vyama vya siasa vimetoa onyo wasitoe rushwa, lakini kwenye mchakato wa uteuzi wameshuhudia ikitembea.

"Tujiulize ni nani waliohongwa kwenye uteuzi, utakuta ni viongozi, kwa kuwa kwenye mikutano ya uteuzi wajumbe wake ni viongozi kuanzia kata hadi halmashauri," alisema.

Warioba alisema hawawezi kumaliza rushwa mpaka wananchi wakatae na kukataa ni mpaka viongozi washawishi.

"Rais Magufuli anahitaji msaada mkubwa ili tufike mahali wananchi wakubali na viongozi wasijidumbukize katika rushwa," alisema.

Alisema ni lazima viongozi wakae pamoja waje na azimio la Arusha ili waweze kukataa rushwa.

"Ajenda ya Rais ya kupambana na rushwa ni nzuri, lakini hali ya kupambana nayo siyo nzuri sana.

"Nina wasiwasi na TAKUKURU kwa sababu ipo chini ya viongozi haitafanya kazi yake vizuri, ninadhani iwe huru ifanye kazi yake bila kufuata maagizo ya kiongozi yeyote la sivyo itakuwa sehemu ya utawala na kupewa maagizo na serikali," alisema.

Alisema Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alipambana na rushwa, hakupokea wala kutoa rushwa.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoa wa Temeke, Donasian Kessy, alisema rushwa ni zao la uozo wa maadili na humsukuma mtu kufanya jambo la uhalifu.

Naye Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mstaafu, Ludovick Utouh, alisema mazingira ya utoaji na mpokeaji rushwa hutokana na hulka ambazo zimegawanyika makundi kadhaa.

Aliyataja kuwa ni ushawishi familia kwa mtu mmoja kuwa na kipato na kuwa tegemezi, hali ya uchumi inayosababisha kushindwa kukusanya mapato, haki ya kisiasa ambayo viongozi wanatokana na rushwa na kukosa uaminifu katika jamii.

Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Prof. Shadrack Mwakalila, alisema lengo la kongamano ni kuenzi na kujifunza yale yote waliyoyaelekeza waasisi wa Taifa la Tanzania.

Prof. Mwakalila amewaeleza washiriki wa kongamano hilo kuwa mada kuu ni mchango wa Mwalimu Nyerere katika mapambano dhidi ya rushwa.


Yetu Microfinance Bank PLC

"Ni yetu ni yako, Pamoja tunaweza"

**YAH: TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA TANO WA WANAHISA WA BENKI YA YETU**

Kufuatia kuahirishwa kwa Mkutano Mkuu wa Tano wa Wanahisa wa benki uliofanyika tarehe 22 Agosti 2020 kwa njia ya mtandao wa "Zoom";

**TAARIFA INATOLEWA KWAMBA,** Mkutano Mkuu wa Tano wa wanahisa wa YETU Microfinance Bank PLC, umepangwa kufanyika tena siku ya **Jumamosi tarehe 29 Agosti, 2020 Msimbazi Center katika Ukumbi wa Holland kuanzia saa tano kamili (5.00) asubuhi.**

**DONDOO:-**

1. Kufungua Mkutano
2. Kuridhia dondoo za Mkutano Mkuu wa tano
3. Kupitia na kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa nne wa wanahisa uliofanyika tarehe 17 Agosti, 2019
4. Kupokea na kujadili yatokanayo na Mkutano Mkuu wa nne
5. Kupokea na kuridhia
   5.1 Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi ya mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2019
   5.2 Taarifa ya Mkaguzi wa hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2019
6. Kuteua Mkaguzi huru wa hesabu kwa mwaka utakaoishia 31 Disemba, 2020.
7. Kupokea na kuidhinisha pendekezo la kulipa Gawio kwa mwaka unaoishia 31 Disemba 2019
8. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
9. Kufunga mkutano

**MAELEZO**

1. Mwanahisa atakayehudhuria Mkutano Mkuu atatakiwa kujigharamia mwenyewe usafiri na malazi.
2. Mwanahisa anayestahili kuhudhuria Mkutano Mkuu ni lazima aje na Cheti cha Hisa cha kumtambulisha kuwa ni mwanahisa pamoja na kitambulisho chake.
3. Fomu ya mwakilishi mbadala (proxy form) itapatikana makao makuu katika jengo la Mkunazini, ghorofa ya pili (2), mtaa wa Kiungani-Kidongo Chekundu na matawini. Fomu husika inayopaswa kujazwa na mwanahisa kwa ajili ya uteuzi huo inatakiwa kufikishwa kwa Katibu wa benki siku tatu kabla ya mkutano.
4. Makabrasha ya Mkutano yatapatikana Makao makuu na Matawi yote ya Benki kuanzia tarehe 25 Agosti 2020 na Ukumbini siku ya Mkutano
5. Wanahisa wote au wawakilishi wao wanahitajika kujisajili kwanza kabla ya kuingia kwenye ukumbi siku ya mkutano.

**Kwa taarifa zaidi tumia anuani ifuatayo:-**

**Katibu**
**Yetu Microfinance Bank PLC**
**Kidongo Chekundu-mtaa wa Kiungani, Jengo la Mkunazini, Ghorofa ya pili**
**S.L.P 75379**
**Dar es Salaam**
**Simu/Fax: 022 2180914; 0655 092 619**
**Baruapepe: info@yetumfplc.co.tz**

**KWA IDHINI YA BODI**
**JOYCELINE KOBERO**

**Katibu wa Benki**
**Tarehe 22 AGOSTI 2020**

**UKIONA TANGAZO HILI MJULISHE NA MWENZAKO**

215869802

# Membe ataja sababu kusaka wadhamini kimya kimya

**Na Enock Charles**

MSHAURI Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo na mgombea urais wa chama hicho, Bernard Membe, ameeleza sababu ya kutafuta wadhamini kimya kimya kuwa ni kuepuka kukosea, hivyo kutengeneza mazingira ya kuenguliwa katika mchakato.

Membe ambaye kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na chama chake hicho kupitia Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Mawasiliano ya Umma, Janeth Rithe, atarejesha fomu hizo katika Makao Makuu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) yaliyopo Njedengwa jijini Dodoma leo, alinukuliwa na chombo kimojawapo cha habari kuwa ameshapata wadhamini 2020 katika mikoa 10.

"Mgombea wa urais wa ACT-Wazalendo, Bernard Membe, amemaliza kutafuta wadhamini 200 wanaotakiwa na tume ya uchaguzi katika mikoa 10 na ameeleza kuwa aliamua kufanya kimya kimya ili kuepuka makosa," alinukuliwa Membe.

Membe ambaye amewahi kuwa Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, alikuwa miongoni mwa wagombea urais kuchukua fomu ya urais NEC akitanguliwa na Rais John Magufuli, ambaye ni mgombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Wengine waliochukua fomu kupambana na Rais Magufuli katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28 mwaka huu ni Tundu Lissu kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Profesa Ibrahimu Lipumba kutoka Chama cha Wananchi (CUF), Yeremia Maganja kutoka Chama cha NCCR-Mageuzi na Hashim Rungwe kutoka Chama cha Ukombozi wa Umma (Chaumma).

Jumla ya vyama 19 vimesimamisha wagombea urais wa Jamhuri ya Muungano, ambapo leo NEC itafanya uteuzi wa wagombea wenye sifa ya kupeperusha bendera za vyama hivyo katika kampeni zitakazoanza kesho.



Kaimu Mkurugenzi wa Uvuvi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ezra Mutagwaba (kushoto), akizungumza katika mkutano wa wadau wa uvuvi uliojadili viwango vya mazao ya dagaa na mwani, jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Rashid Tamatamah na Mratibu wa SWAOFish, Daniel Nkondola. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ndege zote zisizo na rubani lazima kusajiliwa

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), imewataka wamiliki wa ndege zisizo na rubani (drones) kusajili kabla ya Agosti 28, mwaka huu.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TCAA kwenye vyombo vya habari, agizo hilo linahusu ndege zilizopewa kibali awali na ambazo hazijasajiliwa.

"Hatua hii ni utekekezaji wa kanuni za kiusalama za kudhibiti matumizi ya ndege zisizo na rubani ya mwaka 2018, wamiliki wa ndege hizo wanatakiwa kufanya usajili makao makuu ya TCAA," alisema.

Alisema pia wanaweza kusajili katika ofisi za kanda zilizoko Arusha, Dodoma, Iringa, Mwanza, Mtwara, Mbeya, Kilimanjaro, Kigoma, Songea, Tabora, Tanga na Zanzibar.

"Baada ya tangazo hili yeyote atakayekiuka agizo atachukuliwa hatua kali za kisheria. Mamlaka kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wameunda kikosi kazi maalum ambacho kitasimamia utekelezaji wa kanuni," alisema.

Kwa mujibu wa kanuni za udhibiti wa ndege zisizo na rubani za mwaka 2018, zinataka mtu au kampuni kuomba kibali kutoka TCAA kabla ya kuingiza na kusajili, na kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi na serikali za mitaa wakati wa matumizi.

# Bosi TRC awataka w'biashara kupunguza bei ya saruji

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, amewataka wafanyabiashara wakubwa kupunguza bei za saruji, nondo na mabati ili wananchi wajenge kwa gharama nafuu.

Akizungumza jana jijini Arusha na wananchi waliojitokeza kwenye mapokezi ya treni ya abiria iliyofika kwa mara ya kwanza baada ya miaka 30 kupita, Kadogosa alisema treni inasafirisha mizigo kwa gharama nafuu.

"Sasa kama mnasafirishiwa mizigo mikubwa na midogo kwa bei nafuu, ni vema nanyi wafanyabiashara na kampuni za kuzalisha bidhaa mkanufaika na usafiri huu... punguzeni bei za bidhaa zenu ili nao wananchi wanufaike na ujio huu wa treni mkoani kwetu," alisema.

Alisema usafiri huo mkombozi hata kwa wananchi ambao watasafiri kwa Sh.18,000 toka Arusha hadi mkoani Dar es Salaam hivyo kila mmoja anapaswa kumshukuru Rais John Magufuli.

Aliomba wananchi kulinda miundombinu ya reli ili isiharibiwe na inufaishe na vizazi vijavyo.

Mkuu wa Mkoa Arusha, Idd Kimanta, alionya mtu yeyote atakayehujumu miundombinu ya reli atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenan Kihongosi, alisema Rais John Magufuli anahitaji kupongezwa kwa kutoa Sh. bilioni 15 kwa ajili ya kufufua miundombinu ya reli nchini.

Katibu wa Halmashauri Kuu Taifa (NEC) wa Chama Cha Mapinduzi CCM (Itikadi na Uenezi), Humphrey Polepole, alisema ujio wa treni hiyo ni kuidhihirishia Tanzania kuwa CCM wanatekeleza ilani kwa vitendo na sio maneno.

**"Sasa kama mnasafirishiwa mizigo mikubwa na midogo kwa bei nafuu, ni vema nanyi wafanyabiashara na kampuni za kuzalisha bidhaa mkanufaika na usafiri huu... punguzeni bei za bidhaa zenu ili nao wananchi wanufaike na ujio huu wa treni mkoani kwetu," alisema.**

HABARI KITAIFA

# Migogoro ya ardhi Rufiji kuwafukuzisha watendaji

Na Julieth Mkireri, RUFIJI

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, amesema tarafa na kata zitakazobainika kuendelea kuwa na migogoro ya wakulima na wafugaji katika kipindi cha mwezi mmoja, watendaji wake wajiandae kukosa nafasi zao za kazi.

Ndikilo aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wakazi wa Kata za Mkongo na Ikwiriri wilayani Rufiji katika ziara yake ya kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Akiwa katika Kata ya Mkongo, wananchi walilalamikia kuhusiana na uwapo wa wafugaji ambao wamekuwa wakilisha mifugo yao katika mashamba ya wakulima, hali inayoweza kusababisha njaa kwa wananchi.

Seif Lwambo, mkazi wa Kijiji cha Kilimani Kata ya Mkongo, alisema pamoja na mazao yao kusombwa na mafuriko, lakini wafugajj nao wamekuwa chanzo cha kukosekana chakula katika kijiji chao.

"Mafuriko yalipita tukapanda mazao yetu, hawa wafugaji wakaleta mifugo yao wakalisha shambani kwetu, hatuna chakula wao ndio wanatusababishia njaa," alieleza na kuongeza:

"Mnaweza mkahangaika kujenga kituo hiki cha afya, lakini kama suala la wafugaji halitadhibitiwa, hakuna mtu atafika kutibiwa hapa watu watakufa njaa," alisema.

Alimwomba Ndikilo kuhakikisha wafugaji ambao wamekuwa kero kwao wanadhibitiwa ili wakulima walime maeneo makubwa ya kutosha kwa ajili ya kuepuka baa la njaa.

Mbali ya kutoa mwezi mmoja kwa ofisa tarafa wa Mkongo na Ikwiriri pamoja na watendaji wa kata na vijiji kujitathmini kabla hawajafukuzwa kazi kwa kushindwa kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji, aliwataka kutoa ushirikiano kukamatwa wafugaji wanaolalamikiwa.

Ndikilo pia ametoa wiki moja kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Rufiji, Wilbert Siwa, kuhakikisha anamtia mbaroni mfugaji anayedaiwa kumbaka bibi na kumsababishia majeraha.

Katika tukio hilo inadaiwa mfugaji ambaye ni jamii ya Kisukuma alimwingilia bibi huyo bila ya makubaliano ikiwa ni siku chache baada ya mazao yake kuliwa na mifugo.

Ndikilo alitoa fedha za nauli kwa ajili ya bibi huyo kufika kituo cha afya kupata matibabu baada ya kukwama kufika kwa kukosa fedha ya nauli.

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Luteni Kanali Patrick Sawala, alisema atasimamia maagizo yaliyotolewa.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Idd Kimanta (kulia), akinyanyua kiashiria cha kupokea treni ya abiria ya Shirika la Reli Tanzania (TRC), kwa mara ya kwanza jijini Arusha jana, baada ya kutokuwapo kwa huduma hiyo karibia miaka 30 iliyopita. Kulia kwake ni Mwenyekiti wa CCM wa mkoa huo, Zelothe Stephen na Katibu Gerald Munisi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mil. 874/- kuendeleza wabunifu

Na Augusta Njoji, DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imetenga Sh. milioni 874 kwa ajili ya kuendeleza wabunifu wa teknolojia mbalimbali nchini kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Aidha, imesema hadi sasa teknolojia 231 zinazozalishwa vijana wa kitanzania zimetambuliwa kuingizwa kwenye kanzi data ya Taifa.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. James Mdoe, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mafunzo kuhusu masuala ya maendeleo ya teknolojia na ubunifu nchini kwa maofisa maendeleo ya jamii na wathibiti ubora wa shule kwenye mikoa yote ya Tanzania Bara.

Alisema katika kuwaendeleza wabunifu hasa wa ngazi ya chini kwa mwaka 2019/20, wabunifu 1066 wameibuliwa na kutambuliwa na serikali, ambapo kati yao 130 wanaendelezwa na serikali ili ubunifu wao uingie sokoni.

"Na ubunifu wao uwe wa fursa za kiuchumi kwao na uwe mchango kwenye uchumi wa nchi yetu, kwa mwaka 2019/20 serikali ilitenga na kutoa Sh. milioni 750 kwa ajili ya kuendeleza wabunifu," alisema.

Alitaja baadhi ya jitihada zinazofanywa na serikali katika kuwatambua wabunifu ni pamoja na kuandaa mwongozo wa kitaifa wa kutambua na kuendeleza ufumbuzi, ubunifu na maarifa asilia.

"Mafunzo haya yana lengo moja la kuwaleta nanyi tushiriki pamoja nasi na kuhamasisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu," alisema.

Hata hivyo, alisema kuna tatizo la ukusanyaji hafifu wa taarifa za wabunifu kutoka ngazi za kata, vijiji na mitaa na limechangiwa na uelewa mdogo kuhusu dhana ya teknolojia na ubunifu.

Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Wizara hiyo, Prof. Maulilio Kipanyula, alisema lengo la mafunzo hayo ni kurahisisha mchakato wa kuwatambua wabunifu ili wapate fursa ya kuendelezwa.

## Kesi ya 'Mr Kuku' kutajwa Septemba 7

Hellen Mwango

KESI inayomkabili mfanyabiashara, Tariq Machibya (29), maarufu kama 'Mr Kuku' dhidi ya mashtaka saba ikiwamo kujihusisha na biashara ya upatu kwa kukubali na kukusanya Sh. bilioni 17 kutoka kwa umma bila leseni, imepigwa kalenda mpaka Septemba 7, mwaka huu itakapotajwa tena.

Jana kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa dhidi ya mshtakiwa huyo ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Mr Kuku Farmer Ltd, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Janeth Mtega, kwa njia ya Mahakama Mtandao.

Wakili wa Serikali, Esther Martin, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na upelelezi wake bado haujakamilika.

Hakimu Mtega alisema mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu na kesi itatajwa Septemba 7, mwaka huu.

Mapema mahakamani hapo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Simon Wankyo, alidai kuwa Januari 2018 mpaka Mei, mwaka huu, katika mahali tofauti jijini Dar es Salaam, alijihusisha na biashara ya upatu kwa kukusanya fedha kutoka kwa umma.

Ilidaiwa mshtakiwa alikusanya fedha hizo kwa madai ya kufanya ujasiriamali wa ufugaji wa kuku na wangepata faida ya asilimia 70 ya mtaji waliowekeza kwa miezi minne ya awali na asilimia 90 ya mtaji kwa miezi sita kiasi ambacho ni kikubwa kibiashara kuliko mtaji uliowekezwa.

Pia kati ya Januari mwaka 2018 na Mei 2020, maeneo tofauti jijini Dar es Salaam, alikubali na kupokea Sh. bilioni 17 kutoka kwa umma bila kuwa na leseni.

Ilidaiwa, kati ya Aprili 26, 2019 na Januari mwaka 2020 jijini Dar es Salaam, alijihusisha na muamala wa Sh. 6, 477,297,614.83 kwa kuzitoa kutoka kwa akaunti ya Mr Kuku iliyopo benki ya CRDB wakati akifahamu zimetokana na kosa la kujihusisha na biashara ya upatu.

Pia anadaiwa kati ya Januari na Machi 30, mwaka huu, jijini Dar es Salaam, alitakatisha Sh. 629,249,576.36 kwa kuzitoa kutoka akauti ya CRDB wakati akijua zilitokana na kosa la upatu.

Kwamba kati ya Machi 5 na Aprili 17, mwaka huu alitakatisha Sh. 1,366,718,045.46 kwa kuzitoa kutoka akaunti ya Mr Kuku Farmers Ltd iliyopo benki ya CRDB.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Haki itendeke uteuzi wa wagombea uchaguzi 2020*

SASA tunaweza kusema kuwa uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu umeanza rasmi.

Tunasema hivyo kutokana na hatua mbalimbali za awali kukamilika kuanzia uhakiki wa daftari la kudumu la wapigakura, uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa, uchukuaji wa fomu za kugombea kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na urejeshaji wake ulioanza jana.

Jana wagombea urais, ubunge na udiwani kutoka vyama vya siasa 19 walikuwa wakirejesha fomu. Wagombea urais walikuwa wakizirejesha katika ofisi za NEC Makao Makuu Dodoma wakati wagombea udiwani na ubunge kwa wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo husika.

Wagombea hao wamefikia hatua ya kurejesha fomu kwa mamlaka hizo, baada ya kukamilisha masharti yote yanayotakiwa kisheria likiwamo la kukidhi sharti la kuzijaza pamoja na kupata wadhamini.

Baada ya mchakato huo, leo NEC na mawakala wake, ambao ni wakurugenzi wa halmashauri za majiji, manispaa, wilaya na miji watatekeleza jukumu la kuwateua wagombea halali kuanzia leo, kwa maana ya waliokidhi masharti yote yanayotakiwa.

Wagombea ambao watatimiza masharti hayo ndio watakaopeperusha bendera za vyama vyao katika uchaguzi huo, ambao kampeni za kujinadi kwa wapigakura zitaanza kesho.

Tunaelewa jinsi NEC na wakurugenzi watakavyokuwa wakitekeleza kazi ngumu ya uteuzi, ambayo hutawaliwa na malalamiko kutoka kwa vyama, wagombea na wapigakura kwa ujumla.

Wakati wa uteuzi ndipo wadau wa uchaguzi hujitokeza kuweka mapingamizi dhidi ya wagombea, kama sheria ya uchaguzi inavyoelekeza. Wagombea na wapigakura wamepewa mamlaka ya kumwekea pingamizi mgombea yeyote anayeonekana kukosa sifa za kugombea.

Hata hivyo, tunawashauri wahusika kuweka mapingamizi wakiwa na uhakika wa mambo wanayolalamikia dhidi ya mgombea husika, badala ya kuzua tuhuma ambazo hazina ukweli wowote, hivyo kuipotezea NEC muda wa kusikiliza mapingamizi hayo.

Tunaishauri NEC kuwataka watakaopeleka mapingamizi kuwa na ushahidi wa kuridhisha, na ikiona kuna ubabaishaji na malalamiko yasiyo na msingi iyatupilie mbali mapema iwezekanavyo ili mchakato wa kampeni uendelee.

Angalizo hilo tunalitoa kwa kuwa tumekuwa tukishuhudia mara kwa mara wakati wa uchaqguzi baadhi ya wagombea na wapigakura kupeleka mapingamizi yasiyo na msingi, hivyo kuwasababishia usumbufu walalamikiwa na mwishowe tume kuyatupilia mbali.

Tunawashauri wagombea na wapigakura ambao wataamua kupeleka mapingamizi kwa NEC au kwa wakurugenzi wahakikishe kuwa wanakusanya ushahidi na vielelezo vilivyokamilika ili kujenga msingi wa malalamiko yao badala ya kusimamia katika tetesi na ushahidi wa kusikia kutoka kwa wanasiasa.

Itakuwa vizuri kama NEC na wakurugenzi watatenda haki wakati wa kupokea na kusikiliza mapingamizi hayo; kwa maana ya kuwapa muda wa kutosha walalamikiwa kuwasilisha ushahidi wao.

Kwa kufanya hivyo, watajenga mazingira ya kuaminiwa na vyama, wagombea, wadau wa uchaguzi, wapigakura na umma kwa ujumla kwamba wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, kanuni, miongozo na maelekezo ya NEC.


Kwa kutoa maamuzi ya mapingamizi bila kutenda haki ikiwamo kuwashirikisha wahusika wote kunaweza kuibua hisia na malalamiko miongoni mwa wahusika hususan walalamikiwa kuwa hawatendewi haki.

Ni matumaini yetu kuwa NEC itakuwa imejipanga vya kutosha kuhakikisha kwamba kasoro zisizo za lazima hazijitokezi katika hatua hii ya uteuzi wa wagombea.

Tunaamini hivyo kutokana na tume hiyo kukutana na wadau mbalimbali katika hatua za awali kwa lengo la kuweka mambo sawa kuhakikisha kuwa uchaguzi huo unakuwa huru na haki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Elimu ya mpigakura ni muhimu matokeo chanya uchaguzi mkuu

MOJA ya mambo muhimu katika kufanikisha uchaguzi mkuu ni kuwapo kwa elimu ya mpigakura, ambayo lengo lake ni kuwaelimisha wananchi kuhusu mchakato wa uchaguzi ili wawe mstari wa mbele kushiriki kikamilifu.

Dhana hiyo ya elimu ya mpigakura inahusisha hatua mbalimbali ikiwamo usambazaji wa taarifa, vielelezo na vipindi katika njia kuu za mawasiliano vikiwamo vyombo vya habari ili kuwafikia wananchi wengi kirahisi.

Elimu hiyo hutolewa kwa umma ili uzifahamu sheria, kanuni, taratibu za mchakato mzima wa uchaguzi, wajibu na umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi huo.

Aidha, elimu ya mpigakura inalenga kuwahamasisha wananchi kutumia haki yao ya kikatiba, katika kujitokeza na kushiriki kuchagua viongozi watakaowaongoza ili kujenga demokrasia na utawala bora unaowaletea maendeleo endelevu.

Kutokana na umuhimu huo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ikishirikiana na asasi za kiraia katika kuelimisha umma kuhusu mchakato wa uchaguzi kwa kutoa vibali kwa asasi hizo kutoa elimu ya mpigakura.

Lakini, pamoja na juhudi hizo za tume ya kutaka kuhakikisha Watanzania wote wenye sifa washiriki katika uchaguzi mkuu, bado wapo baadhi ambao kila mwaka wa uchaguzi hujiweka pembeni.

Hali hiyo inaonyesha kwamba, inawezekana kuna tatizo ama la kutozingatia elimu ya mpigakura inayotolewa kila mwaka wa uchaguzi au hawafikiwi na elimu hiyo inavyotakiwa.

Kwa mfano, taarifa ya NEC inasema uchaguzi mkuu wa mwaka 2000, wapigakura waliojiandikisha walikuwa 10.9, waliojitokeza kupiga kura wakawa milioni 8.51 sawa na asilimia 84.4.

Uchaguzi uliofuata wa mwaka 2005 waliojiandikisha kupiga kura walikuwa milioni 16.4, lakini waliopigakura walikuwa milioni 11.3 ambao ni sawa na asilimia 69.3.

Mwaka 2010 wapigakura waliojisajili walikuwa milioni 20.1 wakati waliopigakura walikuwa milioni 8.62 mbayo ni asilimia 42.84.

Hali hiyo ya kuendelea kupungua kwa wapigakura haikuishia hapo, kwa kuwa mwaka 2015, kati ya watu zaidi ya milioni 23 walioandikishwa kupiga kura, waliojitokeza walikuwa ni milioni 15.6 sawa na asilimia 67.

Sasa mwaka huu kuna uchaguzi mwingine mkuu, hivyo ni muhimu suala hili la kupungua kwa idadi ya wapigakura likatazamwa kwa kina ili hali hiyo isiendelee kunyong'onyeza demokrasia.

Ni wazi kuwa elimu ya mpigakura inaweza kuchangia kumaliza tatizo hili la kila mwaka wa uchaguzi, hivyo ni muhimu wananchi wakaizingatia, ili kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kuchagua viongozi wanaowataka.

Elimu hiyo inatolewa ili kuhakikisha wapigakura wanahamasika na wanakuwa tayari kwa hiari yao, kwa ufahamu wao na kwa kujiamini kwao kushiriki katika mchakato wa uchaguzi wakiwa na mtazamo wa kukuza demokrasia.

Wakati huu ambao, nchi inaelekea katika uchaguzi mkuu, wananchi watambue kuwa elimu hiyo inawajengea ufahamu na uelewa kuhusu haki na wajibu wao wa kushiriki katika uchaguzi wakiwa na taarifa kamili na sahihi juu za michakato yote ya uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani.

Wataalamu wanaielezea elimu kama uzoefu wenye matokeo ya kujenga akili, tabia au uwezo wa kimaumbile wa mtu binafsi, na kwenye dhana ya kiufundi ikitajwa kama njia ya kupitisha maarifa, ujuzi na maadili kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine.

Kwa mantiki hiyo, elimu inayotolewa kwa wapigakura, waitumie kuhakikisha wanashiriki katika uchaguzi mkuu, badala ya kujiandikisha na kubakia nyumbani siku ya kupiga kura.

Wakati mwingine inakuwa vigumu kuelewa sababu za watu kujiandikisha, lakini siku ya kupigakura hawajitokezi hivyo kuna haja ya kutafuta ufumbuzi na kumaliza tatizo hilo, ambalo husababisha baadhi ya Watanzania kukosa haki yao ya kikatiba licha ya kwamba wamejiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapigakura.

# Upelelezi kesi dhidi vigogo MSD wakaribia kukamilika

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi inayowakabili vigogo wawili wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), akiwamo Mkurugenzi Mkuu wa zamani, Laurean Bwanakunu na mwenzake dhidi ya mashtaka matano ikiwamo kuratibu genge la uhalifu, kusababisha hasara na kutakatisha Sh. bilioni 1.6 umedai kuwa upelelezi wake unakaribia kuiva.

Bwanakunu pia anakabiliwa na shtaka la kutoa nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa MDS bila kibali cha Katibu Mkuu wa Utumishi.

Madai hayo yalitolewa jana na Jamhuri wakati kesi hiyo iliyopangwa kwa ajili ya kutajwa kwa njia ya Mahakama Mtandao, iliyoketi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Janeth Mtega.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Fatuma Waziri, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi wake umefikia hatua nzuri kuiva.

Aliiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Mtega alisema kesi hiyo itatajwa Septemba 7, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Mapema mahakamani hapo Wakili wa Serikali, Faraja Ngukah, alimtaja mshtakiwa mwingine kuwa ni Kaimu Mkurugenzi wa Logistiki wa MSD, Byekwaso Tabura na kuwasomea mashtaka yao.

Katika shtaka la kwanza ilidaiwa kuwa, kati ya Julai Mosi, 2016 na Juni 30, 2019 mahali tofauti jijini Dar es Salaam na nchini wakiwa watumishi wa umma waliratibu genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia faida.

Upande wa Jamhuri ulidai shtaka la pili, kati ya Julai Mosi, 2016 na Juni 30, 2019 katika ofisi za MSD zilizopo Keko Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam washtakiwa kwa pamoja waliisababishia MSD hasara ya Sh. 3, 816,727,112.75.

Ngukah alidai katika shtaka la tatu, kati ya Julai Mosi, 2016 na Juni 30, 2019, ofisi za MDS, Bwanakunu alitumia madaraka yake vibaya kwa kuidhinisha nyongeza ya mishahara Sh. bilioni 3.8 kwa watumishi wa MSD bila kibali cha Katibu Mkuu wa Wizara ya Utumishi.

Katika shtaka la nne, tarehe za tukio, katika ofisi hizo, washtakiwa wote wawili wanadaiwa kushindwa kuhifadhi dawa na vifaa tiba, kitendo ambacho vilikosa ubora na kusababishia MDS hasara ya Sh. 85,199,879.65.

Shtaka la tano, tarehe za tukio katika ofisi hizo, washtakiwa walitakatisha Sh. 1,603,991,095.37, wakati wakijua ni zao la genge la uhalifu.



Makamu Mkuu wa Shule ya St. Anne Marie Academy iliyoko Mbezi Kimara kwa Msuguri, jijini Dar es Salaam, Ambroce Morosso (kulia), akizungumza na wanafunzi wa kidato cha tano shuleni hapo jana, akiwataka kusoma kwa bidii ili kupata matokeo mazuri kama wenzao wa kidato cha sita waliofaulu na kupata sifa za kujiunga na vyuo vikuu katika matokeo ya kidato cha sita yaliyotangazwa mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# DC aagiza watendaji kukamatwa kushindwa kumkamata mhalifu

**Julieth Mkireri, RUFIJI**

MKUU wa Wilaya ya Rufiji, Luteni Kanali Patrick Sawala, ameagiza kukamatwa Mtendaji wa Kata ya Utete, Edmund Chingwile pamoja na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kitundu, Maulidi Tindwa, kwa madai ya kutotekeleza agizo la kumkamata mfugaji anayelalamikiwa kumpiga mkulima.

Alitoa agizo hilo juzi akiwa katika mkutano wa hadhara Mjini Utete, ulioandaliwa kwa ajili ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani kusikiliza kero za wananchi wa wilaya hiyo.

Alisema, viongozi hao aliwaagiza kumkamata mfugaji huyo, lakini hawakutekeleza wala kumpa taarifa ya hatua waliyofikia jambo ambalo alidai kuwa hakufurahishwa nalo.

"Kama wameweza kunidharau mimi hivi hao wananchi watapata haki zao inavyotakiwa, OCD wakamatwe hao viongozi wakae ndani hatuwezi kuvumiliana kwa utaratibu huu," alisema.

Inadaiwa kuwa mfugaji huyo aliyejulikana kwa jina la Lyaga, alimpiga Hassan Kilumbi mguuni na begani.

Akiongea katika mkutano huo Mkuu wa Mkoa wa Pwani Mhandisi Evarist Ndikilo, alimtaka mkuu huyo wa wilaya kuendelea kuwa mkali kwa viongozi ambao wanashindwa kutekeleza majukumu yao.

Ndikilo alisema mtendaji yeyote katika mkoa huo atakayebainika eneo lake kuendelea kuwa na migogoro ya wakulima na wafugaji ndani ya mwezi mmoja hatavumilia kuendelea kufanya nao kazi.

Alisema ni wakati wa watendaji kubadilika na kuachana na tabia ya kufanya kazi kwa mazoea na badala yake wasikilize kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Ndikilo yuko katika ziara ya wilaya za mkoa huo kusikiliza kero za wananchi.

# Matokeo kuwa kipimo utendaji wakuu wa shule

**Na Tiganya Vincent, URAMBO**

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, ameagiza kushushwa vyeo kwa walimu wakuu wa shule ambazo zimekuwa zikifanya vibaya katika matokeo ya mitihani.

Alitoa kauli hiyo jana wilayani Urambo wakati wa mkutano na viongozi na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo kwenye ziara ya kikazi.

Dk. Sengai alisema walimu wakuu wasiokuwa wabunifu wa kuziwezesha shule zao kupandisha ufaulu wa wanafunzi ili waweze kuondokana na daraja sifuri, la nne na tatu hafai kuendelea na nafasi zao.

Alisema ni vema wakaondolewa na nafasi zao kukabidhiwa walimu ambao wako tayari kufanyakazi kwa kujituma na uzalendo ili waweze kuchochea ufaulu katika shule zao na mkoa kwa ujumla.

"Tunaka walimu wale ambao wako 'committed' na willingness na wanafanyakazi kwa uzalendo mkubwa, hao ndio tuendelee kuwafanya kuwa wakuu wa shule, ili waendelee kuwa injini ya ufaulu wa shule zetu," alisema.

# Maofisa mazingira watakiwa kuwajibika

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Usimamizi wa Mazingira Taifa (NEMC), limewataka maofisa mazingira nchini kuwajibika ili kupunguza changamoto ya uchafuzi wa mazingira nchini.

Maelekezo hayo yametolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza hilo, Dk. Samweli Gwamaka, ambaye pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Prof. Esnati Chaggu, wamemaliza ziara ya kutembelea mikoa ya kusini na kuwataka maofisa hao wasimamie ulinzi wa mazingira kutoka ngazi ya kijiji/mtaa, kata, wilaya, manispaa hadi mkoa.

"Kumekuwa na uzembe unaofanywa na maofisa wetu wa mazingira kwenye maeneo mbalimbali nchini kwa kushindwa kutimiza majukumu yao. Wakati umefika kubadilika na kufanya kazi ipasavyo. Watumishi wasipotimiza wajibu wao na ukatokea uchafuzi wa mazingira ni jamii inayotuzunguka pale ndiyo inaathirika," alieleza.

Aliwataka maofisa hao kupeleka ripoti zao ofisi za NEMC na Ofisi ya Makamu wa Rais, Kitengo cha Mazingira kuhusu mazingira ya maeneo wanayoyasimamia nchini na kwamba upelekaji ripoti kunakohusika ni kati ya vigezo vya utendaji wao wa kazi.

"Nawakumbusha maofisa wote wa mazingira kwenye maeneo yote nchini, shirikianeni na NEMC kuhakikisha mazingira ya nchi yetu yanakuwa mazuri na rafiki kwa wananchi," alisema.

# Wizara yaandaa viwango unga wa dagaa na mwani

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi kupitia mradi wa SWIFish kwa kushirikiana na Shirika la Viwango (TBS), wameandaa viwango vya unga wa dagaa na mwani mkavu vinavyoendana na vya kimataifa ili kuongeza thamani ya mazao hayo ndani na nje ya nchi.

Aina ya viwango vilivyoandaliwa ni TBS/AFDC (5714) kwa ajili ya mwani na TBS/AFDC 23 kwa ajili ya unga wa dagaa kwa kuzingatia taratibu za uandaaji wa viwango vya kitaifa ikiwamo kuandaa rasimu na kufanya mikutano ya kamati ya kitaifa ya viwango vya samaki na mazao yake.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayeshughulikia Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, aliyaeleza hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa siku mbili wa wadau unaohusu mjadala wa viwango vya mazao ya mwani na dagaa, ulioshirikisha wavuvi, wafanyabiashara wadogo na wawekezaji.

"Ni matumaini yangu kuwa mwisho wa kikao hiki washiriki na wadau wote watakuwa wameongeza uwezo wao kwa kupitia taarifa mbalimbali zitakazotolewa na hivyo basi kuboresha ubora wa masoko ya zao la mwani na dagaa," alisema Dk. Tamatamah.

Alisema mwani ni zao la biashara linalolimwa katika ukanda wa bahari na hutumika kutengeneza bidhaa za sabuni, sabuni maalum ya kuoshea nywele, vitafunwa na kemikali za maabara.

Katibu mkuu huyo alibainisha kuwa zao hilo linahusisha wakulima 3,000 ambao asilimia 90 ni wanawake na kwa mwaka 2019/20 tani 1.449 zilizalishwa nchini na kati ya hizo, asilimia 90 zilipelekwa China, Marekani, Canada, Uingereza, Denmark na Ufaransa.

Kuhusu zao la dagaa, alisema mauzo ya dagaa kwenda nje ya nchi yanakadiriwa kufika tani 223 zenye thamani ya Sh. bilioni 1.4 kwa mwaka.

Katibu wa Mtandao wa Umoja wa Wanawake wanaojihusisha na uvuvi wa dagaa mkoani Mtwara, Khadija Malibiti, alisema kuanzishwa kwa viwango vya mazao ya mwani na dagaa kutasaidia kuongeza thamani ya mazao hayo, hususan katika utengenezaji wa unga wa lishe unaofaa kuuza nje ya nchi.



Mafundi wakijenga daraja la waenda kwa miguu, eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, ambalo litatumiwa na abiria watakaotoka na kuingia kwenye kituo kipya cha mabasi ya mikoani kinachojengwa eneo hilo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wanahabari wafundwa uchaguzi mkuu Oktoba

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WAANDISHI wa habari nchini wametakiwa wasiwe chanzo cha kuchafua amani kuelekea uchaguzi mkuu, kwani ni vigumu kuirudisha.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Habari Ikulu ya Zanzibar, Hassan Khatib Hassan, alisema, ipo haja kwa waandishi kuepuka ushawishi.

Alisema waandishi wa habari wana mchango mkubwa katika jamii, hivyo wasiwe chanzo cha kuchafua amani na badala yake waelimishe jamii umuhimu wa kuwapo amani hiyo nchini.

"Amani tusiichezee, tuendelee kuilinda kwa sababu mafanikio yote yaliyopatikana ni kwa sababu ya kuwapo kwa amani, hivyo waandishi tusiwe chanzo cha kuivuruga," alisema mkurugenzi huyo.

Alisema kuna baadhi ya waandishi hufanya mambo kwa matakwa yao binafsi, jambo ambalo linaweza kusababisha amani kutoweka.

"Amani ikitoweka sote tutaangamia, hakuna atakayekwenda shamba, kuvua na shughuli zote za kijamii zitasimama, hii ni hatari kwetu, tuchukue jukumu la kuihamasisha jamii idumishe amani," alieleza.

Aliwataka waandishi kushirikiana na Tume ya Mipango katika kuwaelimisha wananjamii juu ya maendeleo yaliyopatikana Zanzibar, ili wajue kwamba serikali inawajali katika kuwapatia huduma stahiki wananchi wake.

Akiwasilisha mada ya Utekelezaji wa Dira 2020, mafanikio na changamoto Mkuu wa kitengo cha ufuatiliaji na tathmini kitaifa kutoka Tume ya Mipango Zanzibar, Jamila Abass Seif, alisema dira hiyo ililenga jamii ambayo itakuza sekta ya kilimo, viwanda, utalii na sekta nyingine za uzalishaji kiuchumi na kijamii ambazo zitakuwa na ushindani utakaoweza kukabiliana na changamoto za maendeleo ya teknolojia za soko la dunia.

## Tamasha la utalii Katavi laja

**Na Neema Hussein, KATAVI**

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, amezindua rasmi tamasha la utalii linalofahamika kwa jina la (Katavi Cultural Tourism Festivals 2020) lenye lengo la kukuza utalii na uwekezaji katika Mkoa wa Katavi.

Homera alisema tamasha hilo lenye kuvutia wawekezaji katika sekta ya utalii linatarajia kufanyika Septemba 25-27, mwaka huu katika viwanja vya Azimio Manispaa ya Mpanda.

Alisema katika tamasha hilo kutakuwa na vitu mbalimbali vya kiasili vinavyopatikana katika mkoa huo, vikiwamo vyakula vya asili, vinywaji vya asili, makumbusho ya vifaa vya kimila, ngoma za asili za makabila ya mkoa wa huo.

Alisema kutakuwa na mashindano ya uchoraji ambapo wachoraji watatakiwa kuchora picha mbili picha moja ya Rais John Magufuli na picha ya pili ni yake (Homera) na washindi watapata zawadi ya fedha na vyeti.

Alisema tamasha hilo pia litahusisha wanafunzi wa sekondari na msingi kwa kuandika insha juu ya uwelewa wao kuhusu utalii na kukuza utalii katika mkoa huo.

## Kafumu ataka CCM kuvunja makundi

**Na Jumbe Ismailly, IGUNGA**

WANACHAMA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora wameshauriwa kuondoa tofauti na kuvunja kambi walizokuwanazo wakati wa kampeni za kura za maoni, badala yake waungane ili ushindi wa wagombea wa chama hicho upatikane.

Ushauri huo umetolewa na aliyekuwa mbunge wa Jimbo la Igunga kwa kipindi cha miaka kumi, Dk. Dalally Peter Kafumu, wakati wa kuwatambulisha wagombea wa ubunge wa Jimbo la Igunga, Nicholaus Ngasa na Seif Khamisi Gulamali wa Jimbo la Manonga baada ya kuchukua fomu za kuomba kuteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Aidha, Dk. Kafumu alifafanua kwamba inawezekana kura za maoni zilikuwa zimewagawa, lakini ni wakati mwafaka sasa wa kuyasahau yaliyopita na wagange yajayo kwani hivi sasa CCM ni moja.

"Ninachowaomba wana Igunga sasa tumemaliza kura za maoni zinaweza kuwa zilitugawa, hebu tuyasahau sasa CCM ni moja, na tutaanza kuanzia Oktoba 28 tuwapige hawa jamaa wa upinzani tupate vijana wetu hawa waweze kuendeleza pale tulipofikia," alisisitiza Dk. Kafumu.

# Red Cross yasaidia shule kukabili magonjwa mlipuko

**Na Yasmine Protace, KIBAHA**

CHAMA cha Msalaba Mwekundu (Read Cross) Tanzania kimekabidhi vifaa vya kujikinga na magonjwa ya milipuko, katika shule za msingi na vituo vya kulelea watoto yatima zilizopo katika wilaya za Mkoa wa Pwani.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Martin Ntemo, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo, Evarist Ndikilo, alisema kuwa msaada huo utawasaidia wanafunzi katika kujikinda na magonjwa ya milipuko.

"Vifaa hivi vitawasaidia wanafunzi kujikinga na magonjwa ya milipuko. Pia unawaji wa mikono umeweza kusaidia hata kudhibitiwa kwa ugonjwa wa corona," alisema.

Alisema jamii inatakiwa kujikinga na magonjwa ya mlipuko kwa kuweka mazoea ya kunawa mikono mara kwa mara.

Alisema wanamshukuru Rais John Magufuli kwa hatua alizochukua katika kipindi cha ugonjwa wa corona na sasa haki imekuwa nzuri ambapo maisha ya Watanzania yamezidi kuendelea kama kawaida kwa kufanya shughuli mbalimbali bila hofu ya ugonjwa huo tofauti na nchi zingine ambazo bado zinapambana na ugonjwa huo.

Mwenyekiti wa Red Cross Mkoa wa Pwani, Stephen Abel Sapi, alisema kuwa wamekabidhi ndoo 100 na mashine 19 kwa ajili ya kunawia mikono katika mkoa huo.

Alisema msaada wa vifaa hivyo ambao umepokelewa mkoani humo, utapelekwa katika shule za msingi na utawasaidia watoto wakiwamo yatima.

Alisema msaada huo, umetolewa katika Mkoa wa Pwani, ambapo shule za wilaya za Kisarawe, Mkuranga, Kibaha Mjini na Vijijini zitanufaika.

**Alisema wanamshukuru Rais John Magufuli kwa hatua alizochukua katika kipindi cha ugonjwa wa corona na sasa haki imekuwa nzuri ambapo maisha ya Watanzania yamezidi kuendelea kama kawaida kwa kufanya shughuli mbalimbali bila hofu ya ugonjwa huo tofauti na nchi zingine ambazo bado zinapambana na ugonjwa huo.**

# Waajiri watakiwa kujifunza kutokana na mlipuko corona

**Na Elizabeth Zaya**

WAAJIRI nchini wametakiwa kujifunza kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona na kuandaa mfumo maalum utakaosaidia wafanyakazi katika taasisi za umma na binafsi kufanyakazi katika mazingira salama hata kunapotokea majanga kama hayo.

Ushauri huo umetolewa na Mkurugenzi wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya Brighter Monday Tanzania, Reshman Shariff, wakati wa uzinduzi wa kitabu kinachotoa mwongozo kwa waajiri nchini.

Shariff alisema lengo la kuzindua kitabu hicho ni kutoa mwongozo bora kwa waajiri namna ya kuwalinda wafanyakazi wao katika vipindi vya majanga na kuwahakikishia usalama wanapokuwa kazini katika vipindi kama hivyo na hata baada.

Pia, alisema kinaangazia hatua muhimu katika mchakato wa namna ya kuajiri, kuweka sera, kufanya maamuzi na kuweka mifumo mizuri ya kufanya kazi kutokea nyumbani bila kwenda ofisini katika vipindi vya majanga.

"Kitabu kimegusia pia masuala ya mawasiliano ya ufanisi na mfanyakazi, usimamizi katika utendaji na ustawi wake, pamoja na mikakati mingine ya kufanya baada ya majanga kama ilivyo kwa corona, na tumeandaa kitabu hiki baada ya kuona utafiti mbalimbali za ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na wataalamu wa taasisi yetu," alisema Shariff.

"Tunakusudia kwamba kitabu hiki kitawasaidia waliopo katika sekta ya usimamizi wa rasilimali watu kwenye taasisi za umma na binafsi katika vipindi vya majanga na hata baada ya majanga hayo na kinaweza kutumika kama mwongozo katika utendaji wa kutengeneza mbinu zinazofaa zaidi katika eneo la kazi."

Alisema ugonjwa wa corona ni janga ambalo dunia haikutarajia na kwamba kuna haja ya kujenga tabia ya kujipanga na mbinu mbalimbali za kusaidia kukabiliana nayo kwa nyakati nyingine.

Alisema kundi jingine ambalo linapaswa kujifunza kupitia mwongozo uliotolewa katika kitabu hicho ni pamoja na wale wanaotafuta ajira.

Meneja masoko wa taasisi hiyo, Erca Uisso, alisema wameamua kutoa kitabu hicho bure ili kusaidia watu wengi na kwamba kitapatikana mtandaoni kupitia tovuti ya Brighter Monday.

Alisema taasisi hiyo imekuwa ikitoa huduma zake katika zaidi ya nchi 10 ikiwamo Tanzania, Kenya, Ethiopia, Uganda, Afrika Kusini, Nigeria, Senegal, Cameroon na Eritrea.



Mwenyekiti wa umoja wa wazaliwa wa Suguti mkoani Mara waishio mikoa mbalimbali nchini, Wakili Said Chiguma, akizungumza katika mkutano wa umoja huo jijini Dar es Salaam juzi, uliojadili mikakati ya maendeleo. Kushoto ni makamu wake, Kusaga Gombania, katibu wa umoja huo, Joseph Jandwa na msaidizi wake, Medard Andrea. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Sekta binafsi yawapa elimu wajasiriamali

**Na Enock Charles**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) imetoa bure elimu ya biashara kwa kikundi cha wanawake wajasiriamali wenye ulemavu wa mwili wa Temeke (UWAVIUTE) jijini Dar es Salaam, ili kuwarahisishia ufanyaji wa biashara, kutunza mahesabu na kutangaza bidhaa zao kupitia mitandao.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Zachy Mbenna, alisema taasisi hiyo ni chombo cha kupazia sauti na kuweka mikakati ya ustawi wa taasisi binafsi ili iweze kufikia malengo ya kuwaunganisha Watanzania na fursa za ndani na nje ya nchi. "TPSF ni chombo cha kupazia sauti na kuweka mikakati ya wadau wake ili waweze kutumia fursa za ndani na nje ya nchi kukuza mitaji yao na kuwafanya wawe na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi," alisema.

Alisema TPSF imeguswa na kikundi hicho cha wanawake wajasiriamali walemavu ambao shughuli zao ni kushona nguo za vitenge, barakoa mashuka pamoja na vitambaa.

"Tumejitolea kusaidia kikundi hiki katika eneo la utoaji elimu ya biashara, utunzaji fedha pamoja na namna ya kutumia mitandao ya kijamii katika kutangaza bidhaa zao ili waweze kupata soko la bidhaa wanazotengeneza," alisema Mbenna.

"Ukuaji wa uchumi wa nchi unategemea sana mchango wa sekta binafsi ambayo huajiri vijana wengi. Tutaendelea kuviunga mkono vikundi vya mfano wa UWAVIUTE kwa kuvipa nguvu ili vitakapoimarika viweze kusaidia vikundi vingine," alisema.

HABARI KITAIFA

# Maofisa ugani wapewa siri ya kuboresha kilimo

Na Hamisi Nasri, MASASI

MAOFISA ugani katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara wametakiwa kufanya kazi kwa kufuata utaalamu wao ipasavyo ili kuendeleza kilimo bora hususan mazao ya korosho na ufuta ambayo ndio tegemezi kwa mapato katika halmashauri hiyo.

Wito huo ulitolewa mwisho mwa wiki na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Changwa Mkwazu, alipokuwa akizungumza na maofisa ugani hao katika kikoa kazi cha maelekezo ya masuala ya kuendeleza kilimo bora.

Alisema asilimia 90 ya mapato kwa wakulima na halmashauri hiyo yanatokana na kilimo hasa cha korosho na ufuta, huku zao la korosho likichangia zaidi ya asilimia 70.

Mkwazu alisema maofisa ugani hao wanatakiwa kutambua kuwa sekta ya kilimo ni muhimu kwa halmashauri kwani fedha nyingi za utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinatokana na mapato yatokanayo na sekta ya kilimo.

Alisema wataalamu hao wa kilimo ngazi ya kata wanalo jukumu la kuwahamasisha na kuwashauri wakulima wote wa korosho kuanzisha mashamba mapya ya zao hilo.

Ofisa kilimo, umwagiliaji na ushirikiano wa halmashauri, Winfrid Tamba, alisema moja ya mkakati wa idara ni kuongeza uzalishaji wa zao la korosho kwa mti mmoja kutoka kilo 10 kwa sasa mpaka kilo 30 kwa mti mmoja.

**Mkwazu alisema maofisa ugani hao wanatakiwa kutambua kuwa sekta ya kilimo ni muhimu kwa halmashauri kwani fedha nyingi za utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinatokana na mapato yatokanayo na sekta ya kilimo.**

# Ruvuma, Mwanza, Tabora zasaidiwa mil. 50/- elimu, afya

Na Mwandishi Wetu, SONGEA

MIKOA ya Ruvuma, Mwanza na Tabora itanufaika katika sekta za elimu na afya kufuatia uwezeshwaji wa shilingi milioni 50.

Uwezeshaji huo umefanywa na Benki ya NMB ambayo imetoa msaada wa vifaa tiba, madawati na mabati vyenye thamani ya Sh. milioni 50.

Misaada hiyo ni mabati 570, madawati 250, mashuka 60 pamoja na vitanda 11, vikiwamo vinne vya kujifungulia.

Kupitia sera ya kutumia sehemu ya faida kusaidia jamii, benki hiyo imechangia mabati 200 kwa ajili ya kupauwa vyumba vya madarasa katika shule za msingi Mlingoti na Nanjoka Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma.

Vifaa vingine vilivyokabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro na meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Janet Shango ni madawati 50 na viti vyake kwa shule ya sekondari Matemanga, vitanda vitano, vikiwamo viwili vya kujifungulia na mashuka 20 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Matemanga. Vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 15.

Akikabidhi madawati 150 kwa ajili ya shule tatu za msingi na mabati 170 za kupauwa Zahanati ya Mitumbati wilayani Tandahima, Shango aliwataka wadau wengine wa maendeleo kujitokeza kusaidiana na jamii kutatua changamoto za miundombinu katika shule, zahanati, vituo vya afya na hospitali za umma. Vifaa vilivyokabidhiwa Tandahima vina thamani ya Sh. milioni 20.

Kwa Mkoa wa Tabora, Meneja wa NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magese, alikabidhi vitanda sita vikiwamo viwili vya kujifungulia na mashuka 40 kwa ajili ya Hospitali ya Nzega Mji. Vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh. milioni 5 vilikabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Nzega, Advera Bulimba.

Kwa Jiji la Mwanza, benki hiyo imetoa mabati 200 kwa ajili ya kuwezeka vyumba vinne katika shule mpya ya Msingi ya Swila inayojengwa kwa nguvu za wananchi, halmashauri na wadau wa elimu.

Akikabidi mabati hayo kwa Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Phillis Nyimbi, pamoja na madawati 50 kwa ajili ya Shule ya Msingi Iseni 'B', Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Baraka Ladislaus, aliahidi kuwa benki hiyo itaendelea kushirikiana na serikali na wadau wengine kuchangia miradi ya maendeleo maeneo mbalimbali nchini.

"Misaada hii ni utekelezaji wa sera ya kurejesha sehemu ya faida kwa jamii; na NMB imetenga zaidi ya Sh. bilioni 1 kwa ajili ya kusaidia miradi ya maendeleo katika sekta ya elimu na afya," alisema Ladislaus.



Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Mkoa wa Pwani, Gulamhussein Shaban Kifu (wa tatu kulia), wakishirikiana kukata utepe kuzindua madarasa mawili, madawati, samani na ofisi za walimu vyenye thamani ya Sh. milioni 57.8 vilivyotolewa na benki ya TPB, katika Shule ya Msingi Kilale, Ikwiriri, mkoani humo juzi. Wengine ni Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Zainabu Ndole (kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Sabasaba Moshingi (wa tatu kushoto), Mkurugenzi wa Majanga, Moses Manyatta (wa pili kushoto), Mkurugenzi wa Masoko, Deo Kwiyukwa (wa pili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msimamizi uchaguzi avipa vyama angalizo

Na Said Hamdani, LINDI

MSIMAMIZI wa uchaguzi Manispaa ya Lindi mkoani humo, Baptista Kihanzi, amewataka viongozi wa vyama vya siasa na wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi wafuate sheria, kanuni na taratibu za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa kujinadi kwa wananchi wanapokuwa majukwaani.

Wito huo aliutoa wakati akikabidhi fomu kwa wagombea ubunge wa majimbo ya Lindi Mjini na Mchinga kupitia vyama vya ACT- Wazalendo na Chama cha Wananchi (CUF).

Wagombea waliochukua fomu Isihaka Rashidi Mchinjta wa ACT- Wazalendo, Salum Bar'wani wa CUF wanaogombea Jimbo la Lindi Mjini na Hamidu Bobari wa CUF Jimbo la Mchinga.

Akizungumza na viongozi na wagombea waliojitokeza kuchukua fomu fomu, Kihanza aliwataka wanasiasa kuhakikisha wanapokuwa majukwaani waendesha siasa za kiustaarabu na sio kutoa maneno ya kashfa dhidi ya wengine kwani kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha kanuni na taratibu za NEC.

Kihanza alisema ni vizuri viongozi na wagombea wanapokuwa wamesimama majukwaani kutangaza sera zitakazowafanya wananchi wavutike nazo, badala ya kashfa na matusi dhidi ya wengine ili kuepuka kubanwa na sheria iliyopo.

"Kama mnavyofahamu kuna uchaguzi wa mwaka huu, kuna sheria zilizowekwa, na ili kujiepusha nazo nyinyi wanasiasa mnatakiwa kuhubiri kwa wananchi sera na sio kashfa," alisisitiza.

Msimamizi huyo alisema kiongozi wa chama au mgombea atakayekwenda kinyume cha maelekezo ya Tume atakabiliwa na adhabu (bila ya kuitaja).

Wagombea hao walimhakikishia kaimu msimamizi huyo wa uchaguzi kuwa watafanya kampeni za kiustaarabu.

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 25, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 12
**Bila sheria mpya itabakia kutwanga maji kwenye kinu**



Ukurasa 14
Maisha bora yalivyojikita kilimohai, viuatilifu asilia



Ukurasa 13
**Usafiri wa anga kurudi mbwa anaponusa virusi vya corona**

ELIMU


**NA BEATRICE PHILEMON**

# Ni habari mbaya mamia wanavyokwama kusoma

IDADI kubwa ya watoto wanaoishi Keko Mwanga B Dar es Salaam, inaelezwa kuwa wanaacha shule na wengine wanachelewa kuanza darasa la kwanza kutokana na kukosa mahitaji ya muhimu ya binadamu.

Wanakosa chakula, daftari, vitabu na matibabu wakiwa wagonjwa, kwa mujibu wa utafiti uliofanyika mwaka 2019 ukihusisha wilaya ya Temeke, wazazi, walezi, kamati za shule na viongozi wa kata ulibaini kuwapo kwa tatizo hilo.

Akizungumza na Nipashe, Meneja Mradi wa shirika la Holt Children Service Incorporation la Korea Kusini, Vaileth Loy, anasema kwa kushirikiana na asasi ya Women In Social Entrepreneurship (WISE), wameanza kuwahudumia watoto hao. Anasema kazi hiyo itafanywa kwenye mradi wa miaka mitatu, unaowalenga watoto 100 wa shule ya msingi kutoka familia masikini.



Mwalimu Baraka Mujunangee, kutoka Shule ya Keko Mwanza, akimfundisha Fahadi Juma, kusoma herufi ndogo wakati wa masomo ya ziada. **PICHA: BEATRICE PHILEMON.**

Anasema kutokana na changamoto hiyo asasi hiyo ya WISE inawasaidia watoto wa kata ya Keko Mwanga B kazi iliyoanza kufanyika baada ya kugundua kuwa watoto wengi hawasomi, wanaacha shule au kuchelewa kwenda shuleni kutokana na hali duni ya uchumi wa wazazi au walezi kushindwa kuwasaidia kusoma.

WISE imeanza kusomesha wanafunzi 88 wa darasa la kwanza japo walilenga wanafunzi 100 wa majaribio wakiwapatia madaftari, sare, vitabu, bima ya afya, chakula, kuwapa masomo ya ziada pamoja na simu janja (vishikwambi 50) kwa ajili ya watoto wanajifunza kwa kutumia mtandao, anasema Loy.

Anaongeza kuwa wana wanafunzi 88 wa darasa la kwanza kutoka kaya masikini wakiwamo yatima, watoto wenye mzazi mmoja , waliotelekezwa, wanaolelewa na babu au bibi, shangazi na wanaotoka kwenye kaya masikini.

Mbali na hilo, pia wakati wa kipindi cha Corona waliwapatia chakula na masomo yao hayakusimama, walifanyakazi za shule nyumbani kila wiki, mzazi anakwenda kuchukua maswali kwenye ofisi ya mtaa na kumsimamia mtoto ayafanye na kuyarudisha ofisi ya mtaa ili walimu wazichukue na kusahihisha na kuzirejesha ofisi ya mtaa ili mzazi azipeleke kwa mwanafunzi.

Jitihada hizo zimesaidia watoto wasisahau masomo na kuendelea kuwa na juhudi kwenye masomo.

"Tuligundua hili baada ya kuwapa mitihani watoto na asilimia mbili pekee ndiyo walishindwa mitihani, kati ya wanafunzi 88 waliofanya mtihani," anasema na kwamba

WISE imesajili walimu watatu kwa ajili ya kufundisha Kingereza, Hisabati na masomo ya sanaa" anaongeza Loy.

**MATIBABU**

Loy anaongeza kuwa kadi za Bima ya Afya (NHIF) zimetolewa kwa watoto 90 wa familia masikini zenye thamani ya Sh. 4,536,000, aidha, kila mwezi familia za watoto hao wanapewa kilo 25 za unga, mchele na maharage kupunguza njaa kwenye familia.

Kwa mujibu wa maelezo yake baadhi ya watoto waliopata bima ya afya wanaumwa moyo, pumu, vidonda vya tumbo, seli mundu (sickle cell anemia) na magonjwa mengine.

Anasema wameamua kutoa kadi za bima ya afya baada ya kugundua kuwa watoto wanachangamoto za afya, hakuna mtu wa kuwahudumia, wengi wanashindwa kwenda hospitali kupata huduma ya afya kwa sababu wazazi wao hawana fedha na matokeo yake mtoto akiumwa anakaa nyumbani bila kupata matibabu kitu ambacho ni hatari kimaisha na kukosa elimu.

Anawahakikishia wanufaika kuwa hiyo ni awamu ya kwanza kutoa bima ya afya na Holt na WISE wataendelea kutoa msaada zaidi kwa watoto katika eneo hili kulingana na mahitaji na fedha kutoka kwa wahisani.

Anasisitiza kuwa wameamua kuanzisha mradi huo baada ya kugundua kuwa watoto wanaacha shule kwa sababu wanakosa mahitaji ya shule kama vile sare, daftari na chakula.

Lakini pia kama wakiumwa wanakosa hela ya matibabu na kusababisha waache shule kwa sababu wazazi na walezi wanashindwa kuwahudumia kupata matibabu lakini pia mazingira ya shule hayavutii.

"Mtoto hawezi kupenda shule kama akirudi nyumbani hakuna chakula wala waangalizi wa kumhudumia, unakuta mama yupo kwenye mihangaiko yake, je, mtoto atapenda kweli kusoma ?" Anahoji.

Loy anaongeza kuwa waligundua kwenye utafiti kuwa wazazi wengi katika eneo hili hawaelewi namna ya kulea watoto na wanajilea wenyewe kwani hakuna anayewafuatilia.

Akizungumza bima ya afya kwa mjukuu wake, Nikolina Nyakung, anasema alishukuru shirika la Holt na WISE kumsaidia mjukuu wake kupata matibabu kwa sababu wakati mwingine mtoto alikuwa anaumwa na kushindwa kupelekwa hospitalini lakini sasa tatizo hilo limemalizika.

Mwenyekiti wa kata ya Keko Mwanga B, Hamza Zayumba, anashukuru WISE na Holt kwa kutoa bima za afya kwa watoto wa familia masikini lakini akaomba pia asasi hizo ziwatazame watu wazima kwa sababu wengi hawana uwezo wa kulipa huduma za matibabu wakiumwa wanabakia nyumbani, jambo ambalo ni hatari kwa maisha yao.

Anasema wengi wanaoishi katika makazi duni, nyumba nyingi ni za urithi na wanaomba kama kuna uwezekano wasaidiwe pia kuboresha makazi yao na kama inawezekana wajengewe upya nyumba kwa sababu zimezeeka.

Aidha, Zayumba anaomba kama kuna watu wanaoweza kuwapatia mitaji ya kufanya biashara wawasaidie ili kupata fedha za kujikimu kiuchumi Hadi sasa kata ya Keko Mwanga B ina zaidi ya wakazi 4,000 wanaoishi katika familia masikini kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kata ya Keko Mwanga B.

ELIMU
NA REUBENI LUMBAGALA

# Bila sheria mpya itabakia kutwanga maji kwenye kinu



Mahudhurio kikamilifu darasani ni muhimu kufanikisha lengo la kujifunza. **PICHA: MTANDAO**

MACHI 2019 gazeti hili lilizungumzia kwa kina jinsi utoro unavyoweza kuchangiwa na sheria ya kudhibiti tatizo hilo, kwani inaelekea kuwa inatoa mwanya kwa watoro kurejea shuleni bila kubanwa.

Katika makala hiyo iliyokuwa na kichwa "Sheria kudhibiti utoro ni kikwazo cha elimu." Iliutaja udhaifu uliopo katika Sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 juu ya suala zima la utoro shuleni.

Uchambuzi ulibainisha namna ambavyo sheria hiyo inavyotoa mwaya mkubwa wa uwepo wa tatizo la utoro sugu mashuleni kwani sheria hiyo inaeleza kwamba mwanafunzi anafutwa shuleni pale ambapo atashindwa kufika shuleni kwa siku 90 mfululizo. (Ni kama miezi mitatu).

Kwa sheria hiyo, mwanafunzi hana hofu anaweza kukaa nyumbani hadi siku 89 mfululizo bila kufukuzwa shule kwa kosa la utoro.

Katika zama hizi za maendeleo na mapinduzi makubwa ya elimu na ushindani wa kielimu, sheria hii haipaswi kuendelea kutumika kwani imepitwa na wakati na haiendani na mazingira na mahitaji na wakati walionao Watanzania.

Kutokana na maendeleo ya elimu, taifa halipaswi kuwa na sheria kama hiyo badala yake ziwepo zinazochochea kasi na maendeleo ya elimu badala ya kuwa na sheria ambazo zinachangia kurudisha nyuma maendeleo ya elimu.

> Tanzania bila utoro mashuleni inawezekana na sheria iboreshwe huku wazazi, walezi na walimu wakitimiza wajibu wao katika mapambano ya kukomesha utoro shuleni.

Utoro wa rejareja na utoro sugu ni miongoni mwa sababu zinazosababisha kurudisha nyuma maendeleo ya taaluma na ufaulu kwa ujumla katika shule za msingi na sekondari nchini.

Hivyo, katika kuhakikisha tatizo la utoro linapungua au kumalizika kabisa, ni wakati wa kuwa na sheria ambazo zitachagiza kutatua tatizo la utoro mashuleni.

Mwanafunzi ambaye anashindwa kuhudhuria kikamilifu shuleni, atakosa kujifunza yale ambayo walimu wameyafundisha darasani tena kwa muda mrefu na hivyo ni dhahiri ufaulu wake wa mitihani utakuwa shakani kutokana na kushindwa kujifunza tena kwa wakati na utaratibu wa kisheria.

Si utoro sugu pekee lakini pia wa 'rejareja' unaofanywa na baadhi ya wanafunzi unawagharimu katika maendeleo yao ya kitaaluma.

Mathalani, mwaka jana, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliagiza kufanywe marekebisho ya sheria hiyo ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978 ili kutatua tatizo la utoro shuleni, lakini hadi sasa marekebisho hayo bado hayajasikika na utoro unaendelea.

Dira ya maendeleo ya nchi inalenga kuifanya Tanzania kuwa taifa la viwanda na la uchumi wa kati, ifikapo mwaka 2025 na tayari mwaka huu 2020 yaani miaka mitano kabla, Tanzania imeshafanikiwa kuwa nchi ya uchumi wa kati.

Kwa hiyo, ili kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa nchi ya uchumi wa kati na baadaye kuwa na uchumi wa juu, ni lazima sekta ya elimu iwe na sheria zinazoakisi dira ya maendeleo na ushindani wa maendeleo uliopo duniani sasa.

Maendeleo ya viwanda na ya uchumi kwa ujumla, yanategemea sana uwepo wa rasilimali watu , wasomi wa ngazi na viwango mbalimbali waliondaliwa vyema katika taasisi za kielimu kuanzia msingi hadi vyuo vya kati na vya juu ili kutumia maarifa, stadi na ujuzi walioupata katika kuchangia maendeleo ya nchi yao.

Pengine ndiyo wakati muafaka sasa kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuharakisha marekebisho ya sheria hiyo ili kupunguza siku ambazo mwanafunzi anaweza kufukuzwa shule kwa utoro kwani siku 90 za sasa ni nyingi mno na zinatoa mwanya wa kuwa na wanafunzi watoro wanaolindwa na sheria.

Walimu wanashindwa kutekeleza kikamilifu malengo yao kwa wanafunzi kutokana na uwepo wa watoro sugu. Mathalani, mwalimu ameazimia kumaliza mada mapema ili aweze kufanya marudio ya kutosha kwa wanafunzi wake na kuinua ufaulu wa somo lake na shule yake.

Katika darasa lake kunakuwa na wanafunzi ambao ndani ya miezi miwili wanafika shule mara moja au mbili, hapa ni dhahiri mwalimu atashindwa kufikia malengo ya kufaulisha wanafunzi wengi kutokana na utoro sugu wa wanafunzi waliopo katika darasa analofudisha.

Serikali imeweka sheria kali kwa watumishi wake kufika kazini kila siku bila kukosa lakini kwa wanafunzi wamekuwa wakilindwa na sheria hii ambayo hakika ni kikwazo cha maendeleo ya elimu nchini.

Naamini serikali itawakumbusha tena Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknojia kuharakisha mchakato wa maboresho ya sheria ya udhibiti wa utoro ili kuwa na siku chache ili wale wanafunzi walio tayari kusoma kwa dhati ya mioyo yao waweze kufahamika mashuleni na kumaliza tatizo la utoro.

Kumalizika kwa tatizo la utoro shuleni kutasaidia sana kufikiwa kwa malengo ya kuinua taaluma yaliyowekwa na viongozi na wadau wa sekta ya elimu kuanzia ngazi ya shule, kata, wilaya, mkoa hadi taifa. Pamoja na umuhimu wa uwapo wa sheria kali ya kudhibiti utoro, wazazi na walezi wawe chachu ya kusimamia kikamilifu watoto wao ili wafike shuleni kama inavyopaswa badala ya wao kuwa sehemu ya tatizo hili kwa kutowafuatilia hasa kwenye mahudhurio na kazi wanazofanya mashuleni.

Tanzania bila utoro mashuleni inawezekana na sheria iboreshwe huku wazazi, walezi na walimu wakitimiza wajibu wao katika mapambano ya kukomesha utoro shuleni.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

***Maoni: 0765-409249.***

SAYANSI

**NA NIMI MWETA**

# Usafiri wa anga kurudi mbwa wanaponusa virusi vya corona




Mbwa aliyefunzwa kunusa majimaji za binadamu kubaini uwapo wa virusi vya COVID-19. **PICHA: MTANDAO**

MATUMAINI ya kurudia hali ya kawaida katika usafiri wa anga yameanza kuonekana baada ya baadhi ya viwanja vikubwa vya ndege kuanza kutumia mbwa kunusa mate na kugundua kwa haraka kama yana virusi vya corona.

Kwa mujibu wa gazeti la NewYork Times, nchi kadhaa zimeingia katika mbio za kutumia mbwa kufanya vipimo vya haraka ambavyo baadhi ya wanasayansi wanasema viko sahihi kwa takriban asilimia 90 kwa hiyo huenda mataifa mengi duniani yakaanza kutumia njia hiyo.

Vipimo vinavyofanyika uwanja wa ndege ni vya kumalizia baada ya kupata tiketi, kama nyenzo ya kusaidia kuthibitisha vipimo vya maabara vya awali.

Baada ya Falme za Kiarabu (UAE) na hasa uwanja wa ndege wa Dubai, Saudi Arabia imeonyesha nia ya kutumia mbwa kunusa mate ya wasafiri au wale wanaoingia nchini kutambua uwepo virusi vya corona.

Taarifa hizo zinasema kuwa Ufaransa,Ujerumani, Chile na Uingereza zilikuwa pia zimeanza mazoezi ya kutumia mbwa kunusa virusi vya corona, hali ambayo inaongeza kwa kiwango kikubwa matumizi ya mbwa katika kuhakikisha usalama viwanja vya ndege.

Mbwa wametumika miaka mingi kunusa mizigo na kujua kama kuna dawa za kulevya, hata kama zimetumika karatasi nene au plastiki kuhifadhi 'unga' wa heroine na sasa wanasaidia katika suala hatari zaidi duniani la corona.

NewYork Times, inasema kuwa Saudi Arabia imefanyia mazoezi aina tofauti za mbwa wa polisi kwa kazi ya kunusa virusi vya corona, wakati ambapo safari za ndege za kimataifa zimeruhusiwa kuanza tena nchini humo.

Taifa hilo linafuatia baada ya Falme za Ghuba kuanza kutumia njia hiyo, kuhakikisha kuwa wasafiri wanaoingia na kutoka wanakuwa salama kwa wenyeji wao, au wakifika wanakokwenda hawatasababisha kueneza virusi vya corona.

Taarifa zaidi zinasema kuwa wataalamu wa kufundisha mbwa hao walitoka katika Taasisi za Kuzuia Magonjwa ya Kuambukiza (CDC) ambazo zina vituo maabara na zinawasiliana kuhakikisha kuwa hakuna tofauti za viwango.

Mkurugenzi wa kituo hicho kwa Saudia alisema majaribio ya kutumia mbwa kugundua watu wenye virusi vya corona yalifanikiwa kwa asilimia 80 hadi sasa kuanzia mwanzo wa wiki ya tatu ya mwezi Agosti.

Inamaanisha kuwa kwa upande mwingine kuwa mafunzo kwa mbwa hao yanaendelea.

Licha ya kuwa mkurugenzi huyo hakutaja ni kiwango gani cha usahihi kinahitajiwa ili njia hiyo iweze kutumika, inaelekea ziko tofauti za ufaulu wa mbwa katika kunusa uwepo wa virusi kwenye mate. Inawezekana pia wasiwe mbwa wote waliopitia mafunzo hayo wanaowekwa uwanja wa ndege kunusa mate, ila wale walioonekana kufikia viwango vya juu zaidi, ambako taarifa nyingine za kitaalamu zinasema usahihi unaweza kufikia hata asilimia 90. Pia ina maana kuwa watakaoshindikana kuonekana wana viwango vidogo sana ambavyo bado 'havitingishi' vipimo nyeti vya mnuso puani.

Utaratibu unaofuatwa Dubai ni kuwa sampuli za mate zinachukuliwa kutoka kwa wasafiri na kuingizwa katika chumba kingine kwa ajili ya mbwa hao kunusa na inachukua dakika moja kubaini kuwepo au kukosekana kwa virusi hivyo.

Kuna baadhi ya utafiti ulifanyika katika nchi tofauti ulioonyesha kuwa mbwa wana uwezo wa kunusa uwepo wa maambukizi kutoka kwenye jasho la mtu, hata kama kwa vipimo vya maabara virusi havikuonekana au hajaanza kukohoa, dalili za mafua na kingine chochote.

Wataalamu wanasema mbwa wana kiwango kikubwa cha kunusa 'hisia' milioni 300 za kupokea harufu, wakati binadamu ana hisia za kunusa 6,000,000, linasema The New York Times.

Nchi za Ghuba na Saudia zinapokea mamilioni ya wafanyakazi kutoka nje kila mwaka ambao wengi walirudi makwao wimbi la corona lilipofika ukanda huo, linaongeza gazeti hilo.

Makisio ya kitafiti ya hivi karibuni yanaonyesha kuwa wafanyakazi wa nje milioni 1.2 walikuwa wanatazamiwa kuondoka Saudia hadi mwisho wa mwaka huu.

Wafanyakazi 150,000 kutoka India walikuwa tayari wameomba nafasi katika ndege za kurudi kwao hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Juni na bado kazi inaendelea.

Takwimu zinaonyesha kuwa Falme za Ghuba zitapunguza nafasi za kasi 900,000 mwaka huu na kuondoa takriban asilimia 10 ya wafanyakazi kutoka nje kutokana na wimbi la kurudi nyumbani lililofuatia kuzuka kwa corona.

Hakuna uhusiano kati ya watu kuondoka na kutokuwepo haja ya kutoa huduma au bidhaa katika mifumo ya uchumi ya nchi hizo mbili, hivyo ikiweza kuhakikishwa kuwa mtu akiingia nchini humo hana corona, au akiingia ofisini wakati wowote, hali inaweza kuanza kuwa shwari.

Hadi sasa majaribio yamehusu kutumiwa mbwa wa kunusa viwanja vya ndege ila teknolojia hiyo lazima itaenea.

> Wafanyakazi 150,000 kutoka India walikuwa tayari wameomba nafasi katika ndege za kurudi kwao hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Juni na bado kazi inaendelea.

Kuna uwezekano vile vile wa kushamiri biashara kadhaa zinazohusika na teknolojia hiyo, kwanza uzalishaji wa mbwa wanaopewa nafasi zaidi ya kunusa virusi vya corona, au ambao ni rahisi zaidi kutumika katika maeneo tofauti.

Shirika moja la utafiti lilitoa taarifa kuwa mbwa walipewa sampuli za wagonjwa makundi mawili, walio na virusi vya corona na wasio navyo, wakafaulu kutoa majibu sahihi bila kukosea.

Kiwango cha ufaulu kwa asilimia 95 katika kugundua sampuli zenye virusi vya corona kilifikiwa na shirika hilo katika taarifa yake ya hivi karibuni.

Baadhi ya wachangiaji katika majadiliano kuhusu matarajio hayo walisema kuwa endapo matumizi ya mbwa kugundua virusi vya corona yataendelea kupanuka, kuna uwezekano shughuli nyingine kama mikutano mikubwa ya wazi na hadhara za kitamaduni au michezo zikaanza kuruhusiwa tena kwenye nchi ambazo zimeanza kufungulia shughuli za uchumi kwa uangalifu mkubwa.

Hata hivyo kuna wasiwasi kuhusu uwezekano wa wanyama kuambukizwa virusi ya corona baada ya mmoja kati ya mbwa wa kundi linalonusa kuambukizwa. Ni maswali yasiyo na majibu ya wazi bado kwa mujibu wa taarifa.

ELIMU

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

# Maisha bora yalivyojikita kilimohai, viuatilifu asilia




Matumizi ya viuatilifu na kemikali za viwandani ni hatari hata kwa viumbe hai wakiwamo wanyamapori. **PICHA: MTANDAO**

WAKULIMA na wafugaji japo wanatumia kemikali kutibu mimea na wanyama wao, wanafahamu fika kuwa matumizi ya kemikali kudhibiti magonjwa ya mimea na ya wanyama ni jambo linaloongeza hasara kuliko tija.

Ndiyo maana kilio cha wengi ni kupata dawa na mbolea za asili ambazo zitakuwa mbadala kwa zile zenye kemikali zinazozalishwa viwandani.

Viuatilifu vya asili ambavyo havitokani na kemikali za viwandani ni muhimu kwa sababu ya ulinzi wa afya za walaji, mazingira na mfumo wa ekolojia.

Licha ya kusisitiza umuhimu kwa wakulima kusaidiwa kupata dawa hizo kudhibiti magonjwa, lakini pia ni bora zaidi wakaelezwa kwa kina umuhimu wake kwenye kutunza afya zao, mazingira na bayoanuai.

Licha ya kwamba wakulima wanatumia dawa ambazo zinaondoka haraka kwenye mazingira ambazo hunyunyuziwa kwenye mimea hasa mboga na matunda, lakini matumizi yake hayafanyiki kwa usahihi kutokana na kupuliziwa kwenye mmea muda mfupi na mazao kupelekwa sokoni yakiwa na sumu. Ili kuondoa tatizo hilo ni vyema kutumia viuatilifu vya asili.

Dawa mbalimbali hutumika kwenye kuzalisha mazao. Ili yawe na tija ndiyo maana inatakiwa kufanyiwa utafiti kufahamu kiwango cha 'sumutiba' ambacho kinaweza kuua au kudhibiti wadudu katika mimea.

> Kinachohitajika sasa ni utafiti wa dawa hizo zisizo na kemikali na matokeo yake yafikishwe kwa wakulima ili wanufaike na kilimo hai kinachookoa mazingira.

Lakini, pia kufahamu athari zake kwa afya na mazingira ili kujua iwapo kuna tija ama hasara kiafya kwa mlaji na mazingira yake.

Mathalani, mwarobaini, ambao anaeleza kuwa umeshafanyiwa utafiti na kugundulika kuwa unaweza kudhibiti baadhi ya wadudu kwenye mimea na wanyama ni vyema dawa kama hiyo ikatafitiwa ikatumiwa na wakulima katika maeneo mbalimbali kukabiliana na magonjwa na wadudu waharibifu.

Lakini, kinachoshangaza ni kukosekana kwa tiba hizo kwenye maduka ya dawa na badala yake kuendelea kupatikana viuatilifu vya viwandani zaidi na hata kuibuliwa kwa matoleo mapya kila wakati.

Aidha, dawa kama aloivera nayo inatajwa kuwa inapochujwa na kuandaliwa kitaalamu ni dawa ya kutibu magonjwa ya mimea, wanyama hasa ndege.

Halikadhalika, mkojo wa sungura nao unaelezwa kuwa ni miongoni mwa vitu vinavyoweza kutumiwa kupata dawa bora au viuatilifu vinavyoangamiza wadudu au visumbufu kwenye mazao. Lakini, kote changamoto ni moja upatikanaji madukani. Bidhaa hizo hazionekani.

Zama hizi yameibuka matumizi ya 'booster' inayolezwa kuwa ni mbolea mbadala inayozalishwa viwandani ambayo inapowekwa kwenye mimea inawezesha mizizi kufyonza chakula , majani na shina kufyonza virutubisho na maji vilivyoko ardhini kwa urahisi ikiwa ni pamoja na mbolea iliyoko ardhini.

Booster inatajwa kuwa ina uwezo wa kuiongezea mimea uwezo wa kufyonza na kuchakata virutubisho vyote kwa kasi na pia inapunguza matumizi ya mbolea za viwandani na pia kuongeza kasi ya ukuaji, huipa mimea afya zaidi kuongeza mazao, kuyapa ladha bora na huishi muda mrefu au huyaongezea zaidi imani.

Kinachohitajika sasa ni utafiti wa dawa hizo zisizo na kemikali na matokeo yake yafikishwe kwa wakulima ili wanufaike na kilimo hai kinachookoa mazingira.

Wakati huu wakulima wanatumia dawa za 'booster', kuna dawa aina mbali mbali na kundi la kwanza ni zile ambazo zinapoingia ardhini au kwenye maji zinadumu kwa miongoni nazo ni kama DDT ambayo inaelezwa kutumiwa kutibu malaria.

Inadaiwa DDT ni chanzo cha wengi kupata saratani, wanyama na mimea wanaathirika pia kuku ni miongoni mwa wanyama walioumizwa na kemikali hiyo kwa vile walitaga mayai yenye kaakaa laini na hayakuweza kuanguliwa. Hata kama yaliliwa ni sawa na kula sumu hiyo. Nyakati hizi dawa hiyo haiko kwenye soko lakini inatumika kwenye uzalishaji wa mboga na kutibu mazalia ya malaria.

Wanadamu na wanyama wanapokula dawa kama hizo sumu yake inahifadhiwa kwenye seli za mafuta na jinsi muda unavyokwenda zinaleta madhara yanayotishia maisha na hata kifo.

### ILIPO HATARI

Pamoja na sumu zinazonyunyiziwa kwenye mimea kuna mbolea zinazowekewa ama kuikuza au kupandia nazo zina kemikali ambazo, wakati mwingine huendelea kuleta athari kwa watumiaji na mazingira.

Wapo wakulima ambao humwagilia mbolea ya chumvichumvi kwenye mazao na kuyauza muda mfupi baadaye, jambo linalosababisha wateja kula mbolea hiyo ambayo haijachakatwa na kufyonzwa na mmea hali inayotishia afya za wengi wakiwamo watoto, wajawazito na wazee.

Itakumbukwa kuwa mazao na wanyama yanayolimwa na kufuga kwa kutumia mbolea za viwandani ni mengi lakini athari zipo kwenye mazao ya muda mfupi kama mboga, matunda na wanyama kama kuku na nyuki.

Kupunguza matumizi ya viuatilifu vya viwandani kulenge kuinua kilimo hai au cha kijani ili kuboresha afya za watu na mazingira kwa kuzingatia ufugaji na ukulima usiotumia kemikali za sumu.

Kama kilimo na ufugaji utakuwa unategemea zaidi kemikali ni wazi walaji hawatakuwa salama na mazingira hayatalindwa. Afya za walaji haziwezi kuwa kamilifu na kinachohofiwa ni ongezeko la saratani za viungo mbalimbali na magonjwa mengine mengi yasiyotibika.

Kwa hiyo zinahitajika jitihada kuwa na viuatilifu na mbolea zinapotumika kuzalisha vyakula ni vyema kuhakikisha udongo unaachwa ukiwa salama, lakini pia dawa zinatumiwa hazichafui vyanzo vya maji yawe yanayotiririka kwenye mito au ya kwenye maziwa au baharini na yoyote yale hata kama itakuwa ni yale yanayotumiwa viwandani au ya madimbwi, na kwenye malambo yanayotumiwa na wanyama au kumwagilia mazao mbalimbali.

Kulima kuboreshe ardhi na kupata chakula cha kutosha na kisicho na kemikali za sumu. Kutumia dawa za viwandani ni gharama kubwa na matokeo yake ni kuleta madhara ya kiafya lakini kemikali za asili kama alizeti pori, pilipili kichaa, majivu na hata wakati mwingine mkojo wa sungura na ng'ombe hakuna athari.

Dawa za asili kama vile mwarobaini , mkojo wa ng'ombe na alizeti pori zinatumika kwenye uzalishaji wa mahindi kwa kutumia mbolea ya samadi kunalinda mazingira na wadudu kama vipepeo na ndege wanaendelea kuzaliwa kwenye mazingira salama.

Kama pia mimea itakuwa salama ni dhahiri nyuki wanachavusha na kuishi kwenye mimea salama kwa vile hata asali ambayo ni dawa bora inatishiwa kutokana na matumizi ya kemikali za sumu zinazojaa ardhini na angani.



## HABARI DODOMA

# Waziri Mavunde aomba kuombewa

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

MBUNGE wa Dodoma Mjini ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, amewataka wananchi kumwombea ili asiangukie mikononi mwa shetani kwa kuwa na kiburi cha fedha na madaraka.

Mavunde, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waumini wa kanisa la Pentekosti Agizo Kuu lililopo Ndachi jijini Dodoma, wakati wa harambee ya ujenzi wa kanisa, kituo cha kulelea watoto wadogo na shule ya awali.

Pia pamoja na kuwaomba wananchi wa Dodoma kumwombea aliwataka Watanzania, kuendelea kuliombea taifa ikiwa ni pamoja na kuombea uchaguzi ili uwe huru na haki. Aidha, Mavunde alisema kuwa Tanzania ni kati ya mataifa ambayo yanatamaniwa na nchi nyingine kutokana na kuwa na amani, upendo na utulivu.

"Tofauti na ujenzi ambao unaendelea, lakini wananchi tunapaswa kuiombea nchi yetu pamoja na viongozi wa nchi akiwamo Rais wa Jamhuri ya Tanzania, Dk. John Magufuli," alisema Mavunde.

Kwa upande wake, Askofu Mkuu wa Kanisa la Pentekosti Agizo Kuu, Dk. Dismas Mukasa, alisema kuwa kanisa lina jukumu kubwa la kuwahudumia watu kiroho na kimwili.


Alisema kanisa hilo linatimiza wajibu wake kwa kuhakikisha jamii ya Watanzania wanahudumiwa kwa njia iliyo salama kwa kutimiza maandiko.

Dk. Mukasa ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM Mkoa wa Dodoma, alisema pamoja na mambo mengine kanisa lake linaendelea kufanya maombi kuliombea taifa pamoja na uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 2020.

Akisoma risala katika harambee hiyo Mariam Edmund, alisema kuwa hadi ujenzi huo unakamilika itagharimu kiasi cha Sh. milioni 400.

Hata hivyo, alisema kanisa halitegemei wafadhili bali washirika wa kanisa hilo wamekuwa wakijitolea kuendelea kujenga kwa kutoa mali na fedha kwa nguvu zao.

"Tunategemea kujenga kanisa, nyumba ya kutunzia watoto pamoja na shule ya awali ili kukamilika ni lazima zipatikane Sh. milioni 400," alieleza.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. bilioni 16 kwa Ofisa wa Mambo ya Uchumi wa Ubalozi wa Uholanzi nchini, Mathijs van Eeuwen (kushoto), iliyotolewa na Benki ya NMB gawio kwa Rabo Bank Group, jijini Dodoma. Wengine (kutoka wa pili kushoto) ni Msajili wa Hazina, Athumani Mbuttuka, Mjumbe wa Bodi ya NMB, Magreth Ikongo, Mwenyekiti wa Bodi, Dk. Edwin Mhede na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Ruth Zaipuna. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hospitali ya Mkapa yapigwa jeki vifaa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa (BMH) imepokea msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 2, kwa ajili ya watoto wenye matatizo ya kupumua kutoka chama cha wakunga nchini (TAMA).

Vifaa hivyo aina ya Penguine Suction, hutumika kuondoa uchafu kwenye pua na mdomo kwa mtoto mchanga baada ya kuzaliwa.

Mkurugenzi wa uuguzi wa BMH, Salome Kassanga, alisema vifaa hivyo ni muhimu kwa sababu husaidia kunyonya maji kwa watoto wanaokunywa maji wakati wa kuzaliwa ili kuwaepusha na vifo.

Kassanga alisema baada ya mtoto kuzaliwa, hulazimika kunyonya maji hayo kwa kutumia kifaa maalum ili kunusuru maisha ya mtoto huyo kwani maji hayo huziba njia ya hewa.

Kassanga alisema mtoto aliyekunywa maji wakati wa kuzaliwa anapaswa kunyonywa maji hayo kwa haraka ili kuzibua mfumo wake wa hewa kwani akiachwa kwa muda mrefu huweza kupoteza maisha.

Alisema unyonyaji maji hayo kwenye mdomo na pua za mtoto hutakiwa kufanyika kwa haraka na wakunga pale tu mtoto anapozaliwa na kuonekana amekunywa maji hayo yanayomsababisha ashindwe kulia na kupumua vizuri.

Alisema vifaa vya kuwasaidia kunyonya maji hayo kwenye mdomo na pua za watoto wachanga ni muhimu kuwapo kwenye wodi za wazazi ili kunusuru maisha ya watoto waliokunywa wakati wa kuzaliwa.

Mkurugenzi huyo alisema kwa wastani hospitali hiyo huzalisha wanawake 200 kwa mwezi, hivyo wanatakiwa kuwa na vifaa hivyo vya kutosha ili kuhakikisha kuwa kila mtoto anayezaliwa na tatizo hilo anahudumiwa kwa wakati.

Alisema hivi karibuni hospitali hiyo ilikuwa inahitaji kuongeza vifaa hivyo, lakini upatikanaji wake ulikuwa ni mgumu kwani walikuwa wanalazimika kuagiza kupitia bohari ya dawa nchini (MSD) ambapo nako vilikuwa havipatikani.

Alisema hospitali hiyo ni tawi la TAMA, ambapo walipowatembelea waligundua kuwa hospitali hiyo ilikuwa na vifaa vichache vya kunyonyea maji kwa watoto wachanga, hivyo kuwapatia vifaa vingine ili kukidhi mahitaji.

"Siyo kwamba hatukuwa na vifaa hivyo, vilikuwapo, lakini vilikuwa ni vichache na hata hospitali ilipoagiza MSD vilikuwa havipatikani, hivyo chama cha wauguzi kwa kuwa walikuwa navyo walitulea kwa ajili ya kutoa huduma kwenye mazingira mazuri."

"Ni kawaida kwa chama cha wakunga kutembelea matawi yao na kuangalia mapungufu yaliyopo ili kuwasaidia wakunga nchini kufanya kazi kwenye mazingira rafiki kwa kuwa na vifaa vyote vinavyohitajika kwenye kazi yao ya ukunga," alisema Kassanga.

Akipokea msaada huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika, ameishukuru TAMA na UNFPA kwa vifaa hivyo, ambavyo ni mkombozi kwa kinamama, watoto na wakunga.

## SIDO yanoa wajasiriamali utunzaji fedha

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini (SIDO) mkoani Dodoma, limetoa mafunzo ya namna ya utunzaji fedha ikiwamo kujiajiri kwa vijana 45, kutoka vikundi mbalimbali vya ujasiriamali katika Halmashauri ya Chamwino mkoani Dodoma.

Mafunzo hayo yametolewa na SIDO kwa kushirikiana na mtandao wa mazingira Dodoma (DONET) na yamefanyika kwa siku nne.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, ofisa uendelezaji wa biashara kutoka SIDO Dodoma, Chrispin Kapinga, alisema lengo la mafunzo ni kutaka kuwafundisha vijana namna ya kutunza fedha, lakini kujiajiri wao wenyewe pasipo kusubiri ajira toka serikalini.

"Tumefanikiwa kutoa elimu kwa vijana, lakini zoezi hili litaendelea katika maeneo mbalimbali hapa jijini Dodoma," alisema Kapinga.

Kapinga alisema lengo lao ni kuona vijana wanakuwa mstari wa mbele kuleta maendeleo katika taifa hasa hivi sasa linapoelekea katika uchumi wa viwanda.

"Vijana wanahitaji kuchangamka taifa lilipo sasa kwenye uchumi wa kati linahitaji vijana wachapakazi na sio kubweteka," alisema Kapinga.

Alisema lengo lao ni kuona kila kijana ana mafanikio makubwa kupitia kujiajiri yeye mwenyewe.

Kapinga alisema ndani ya siku nne vijana wametoka na kitu ambacho kitakwenda kuwasaidia katika maisha yao na ujasiriamali wanaofanya katika maeneo mbalimbali.

Naye Emmanuel James, mratibu wa kuwawezesha vijana kukamata fursa za kiuchumi DONET, alisema mafunzo hayo yamekuwa na manufaa makubwa kwa wajasiriamali kwa sababu itawasaidia katika biashara zao.

James, alisema taifa hivi sasa linakwenda kasi kutokana na serikali iliopo madarakani kuhitaji watu wachape katika ajira, ndio maana wao wanajitahidi kuwapa elimu vijana ili wasibweteke kusubiri ajira.

Alisema lengo lao ni kuwainua vijana wa Dodoma ili wajiajiri wao wenyewe na sio kusubiri ajira wakati kazi za kufanya zipo.

Kwa upande wake Emmy Godfrey kutoka kikundi cha ujasiriamali cha Upendo, alisema wamenufaika na mafunzo hayo na watakwenda kuyafanyia kazi ipasavyo.

Alisema awali walikuwa hawana elimu hiyo, lakini hivi sasa wameipata na watakwenda kuifanyia kazi katika vikundi vyao vya ujasiriamali.

Naye Sofia Swai, mratibu wa vijana na mashirika yasiyo ya kiserikali, aliwataka vijana kwenda kutumia mafunzo waliopata vizuri ili wajiendeleze.





## Mgombea achukua fomu, aahidi kampeni kistaarabu

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Oran Njeza, amekabidhiwa fomu ya kuwania nafasi hiyo na Msimamisi Msaidizi wa uchaguzi, Steven Katemba, huku akiahidi kufanya kampeni za kistaarabu.

Njeza ambaye kabla ya mchakato wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu kuanza, alikuwa mbunge wa jimbo hilo, alichukua fomu hiyo mwishoni mwa wiki na kuishukuru serikali kwa kuzuia mbwembwe wakati wa kuchukua fomu hizo ikiwamo maandamano.

Alisema utaratibu huo unasaidia kuimarisha demokrasia ndani ya taifa kwa maelezo kuwa kuzuia idadi kubwa ya watu kwenda kumsindikiza mgombea kuchukua fomu wakati kampeni hazijaanza na haileti picha nzuri.

Alisema alipitishwa na vikao mbalimbali vya chama hicho kuwa mgombea kwenye uchaguzi wa mwaka huu kutokana na kutekeleza vizuri ahadi zake wakati wa awamu yake ya kwanza pamoja na uadilifu wake ikiwamo kutokuwa mla rushwa.

"Ukiona umeteuliwa na CCM ujuwe umepita kwenye tanuru la moto, hivyo mimi naamini viongozi wa chama akiwamo Mwenyekiti wetu Rais Magufuli waliridhika na uwezo wangu," alisema Njeza.

Alisema baada ya kampeni kuzinduliwa atawaeleza wananchi ahadi zake baada ya zile alizokuwa ameahidi mwaka 2015 kuzitekeleza kwa asilimia kubwa ikiwamo utekelezaji wa miradi ya maji ambayo tayari wananchi wameanza kunufaika nayo.

Alisisitiza kwa kuwa sasa hivi Tanzania imeingia kwenye uchumi wa kati, Watanzania wanatakiwa kufanya maamuzi sahihi ambayo yatasaidia uchumi huo kuzidi kuimarika zaidi pamoja na uboreshaji wa miundombinu.

Njeza alisema kwa sasa serikali imeanza utaratibu wa kuboresha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA), ili kuwarahisishia wananchi usafiri na usafirishaji wa mazao yao kwenda kwenye masoko.

# Askofu ahamasisha Watanzania kupiga kura

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

WATANZANIA wameshauriwa kujitokeza kupiga kura kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na madiwani unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu, ili kuwachagua viongozi watakaosaidia kuwaletea maendeleo.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Askofu Mkuu wa Kanisa la Moravian Tanzania Jimbo la Kusini Rungwe, Kenan Panja, wakati wa harambee ya kuchangia ujenzi wa Kanisa la Moravian, Ushirika wa Kyela mkoani Mbeya.

Askofu Panja alisema, kupiga kura ni haki ya kila Mtanzania na hivyo akawataka wananchi kutekeleza haki hiyo kwa vitendo hasa kwa wale ambao walishajiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Alisema kila Mtanzania mwenye sifa za kupiga kura anatakiwa kushiriki huku akiwataka viongozi wa dini kuendelea kuwahamasisha waumini wao kushiriki kwa kuwa uchaguzi huo ndio tafsiri halisi ya demokrasia.

"Mwaka huu ni wa uchaguzi na kwa mujibu wa kalenda ya taifa, uchaguzi huo utafanyika Oktoba 28, sasa nawaomba Watanzania wote tushiriki zoezi hilo kwa amani na utulivu ili tupate viongozi watakaotuongoza kwenye shughuli za maendeleo," alisema Askofu Panja.

Mwenyekiti mstaafu wa kanisa hilo, Clement Mwaitebele, alisema Rais Dk. John Magufuli, amefanya kazi kubwa ya kuwafundisha Watanzania kujitegemea kiuchumi na kuachana na utegemezi wa misaada yenye masharti magumu.

Alisema hata makanisa kwa sasa yameanza kujifunza kujitegemea tofauti na ilivyokuwa awali na madhehebu mengi yalikuwa yanategemea misaada kutoka nje ya nchi ambayo baadhi ilikuwa na masharti.

Mwaitebele alisema kwa muda mrefu Watanzania walikuwa wamelala na kulikuwa hakuna matumaini ya kuweza kujitegemea, lakini kwa sasa utekelezaji wa miradi mingi kwa kutumia mapato ya ndani umeanza kuwaamsha.

"Magufuli amesaidia kutubadili 'mindset' (fikra), elimu aliyotupa kwa kweli imetusaidia na nawapongeza Watanzania hasa waumini wa madhehebu mbalimbali wameitikia vizuri elimu anayotoa, sasa hivi makanisa yanajitegemea kwenye ununuzi wa mali mbalimbali," alisema Mwatebele.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Kanisa hilo, Sem Mwakaje, alisema walitisha harambee hiyo kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kanisa hilo bila kuomba misaada kutoka nje ya nchi na badala yake wapate michango ya Watanzania.

Alisema kwenye harambee hiyo walikusudia kupata Sh. milioni 40 ambazo zingeweza kukamilisha ujenzi wa kanisa hilo na kuwaomba waumini wa kanisa hilo kuendelea kujitolea kwa hali na mali.

Mwasisi wa ujenzi wa kanisa hilo, Mchungaji Musa Mwakabelele, alisema tangu kuanza kwa ujenzi wa kanisa hilo walikuwa wanategemea misaada kutoka kwa wazungu, lakini kutokana na masharti waliyokuwa wanapewa waliamua kuachana nayo na kuamua kujitegemea.

Aliwataka Watanzania kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo wenyewe na kuwa na uwezo wa kuendesha miradi kwa fedha za ndani.





Mgombea ubunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza (kushoto), akikabidhiwa fomu ya uteuzi wa kuwania nafasi hiyo na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Steven Katemba, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Walimu wa kujitolea kupewa kipaumbele ajira

**Nebart Msokwa, MBEYA**

UONGOZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, umesema utawapa kipaumbele cha ajira walimu ambao wanajitolea kufundisha shule mbalimbali za sekondari ndani ya halmashauri hiyo bila malipo endapo serikali itatoa fursa hiyo.

Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri hiyo, Aliko Mbuba, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa utekelezaji wa mradi wa kikundi cha walimu wa kujitolea kufundisha shule za sekondari za serikali katika halmashauri hiyo kiitwacho COFAPS.

Alisema endapo itatokea fursa ya ajira za walimu, majina ya walimu wa kujitolea yatapelekwa katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili waajiriwe kwa kuwa wameonyesha moyo wa kujitolea.

Alisema halmashauri hiyo inakabiliwa na tatizo la upungufu wa walimu na kwamba uwepo wa walimu wa kujitolea umesaidia kukabiliana na tatizo hilo hasa kwa masomo ya sayansi ambayo ndiyo yana uhitaji mkubwa wa walimu kwa sasa.

"Moja ya matatizo ya walimu hawa ni ajira, wamejitolea kwa muda mrefu hata kabla ya kuzuka kwa ugonjwa wa virusi vya corona, walikuwa wanajitolea, sasa ili kuwasaidia tutapeleka majina ya walimu hawa TAMISEMI, ili wapewe kipaumbele cha ajira," alisema Mbuba.

Alisema walimu hao wanaojitolea wameonyesha uzalendo wa hali ya juu na hivyo ikitokea wakapata upendeleo haitakiwi mtu yeyote kuibua maneno ya kuonyesha kuwa wamependelewa.

Akitoa taarifa ya kikundi hicho, Calory Mirambo, ambaye ni katibu wa kikundi cha COFAPS, alisema kikundi hicho kilianzishwa mwaka 2017 na walimu saba ambao walikuwa ni wahitimu wa shahada ya ualimu kutoka katika vyuo vikuu mbalimbali nchini na kwamba jina la kikundi linatokana na kifupisho cha majina ya waanzilishi hao.


Vilevile alisema kikundi hicho kina lengo la kuwajengea uwezo na uzoefu walimu waliopo mitaani ambao bado hawajapata ajira serikalini ili wawe na sifa za ushindani katika soko la ajira ndani na nje ya nchi.

"Kikundi hiki cha COFAPS mpaka sasa kina jumla ya walimu 41 ambao tayari wamesambaa katika shule mbalimbali za serikali ili kuendeleza mradi, lakini kuna walimu 19 ambao wanasubiri kupangiwa shule za kwenda kujitolea kufundisha," alisema Mirambo.

Hata hivyo, alisema kikundi hicho kimefanikiwa kuzifikia kata tano kati ya sita ambazo walilenga kufanya kazi ambazo ni Bonde la Usongwe, Utengule -Usongwe Nsalala, Iwindi na Kata ya Ijombe na kwamba kata ya Igale mpaka sasa hawajaifikia na wanaendelea na harakati za kuifikia.

Alisema shule nane zilizopo kwenye kata hizo ambazo ni Shule ya Sekondari Ilunga, Iwindi, Mwaselela, Usongwe, Songwe Sekondari, Malama, Iwalanje na Nsongwi Juu.

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Utengule- Usongwe, Costalika Mdapo, alisema kabla ya mradi huo kuanza, shule hiyo ilikuwa na uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi na kwamba mpaka sasa wanafunzi wanaendelea kunufaika na matunda ya walimu hao.





## Wanaofanya uvuvi haramu sasa kukiona

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja, Rajab Ali Rajab, ameiagiza kamati ya uvuvi Shehia ya Kiwengwa kuwachukulia hatua za kisheria wavuvi wote ambao watashindwa kufuata taratibu na sheria za kamati hiyo kwa kujihusisha na uvuvi haramu.

Alisema idara ya uvuvi imekuwa ikishirikiana na kamati za uvuvi katika shehia kwa kutoa elimu kuhusu athari za uvuvi haramu, lakini bado kuna baadhi ya wavuvi wamekuwa wakikaidi maelekezo hayo na kusababisha uharibifu wa mazalia ya samaki (matumbawe) na viumbe vya baharini.

Akizungumza juzi na baadhi ya wajumbe wa kamati ya uvuvi Shehia ya Kiwengwa pamoja na wavuvi kutoka Shehia ya Matemwe ambao wamekuwa wakijihusisha na shughuli za uvuvi kwa kutumia nyavu za macho madogo, Mkuu huyo wa Wilaya alisema eneo la Kiwengwa ni eneo la hifadhi, hivyo ni vyema sheria na taratibu za uvuvi zikazingatiwa.

Naye Ofisa Uvuvi Wilaya ya Kaskazini 'A', Nhoda Khamisi Kheir, alisema katika maeneo ya hifadhi uvuvi wa nyavu za macho madogo hazitakiwi kutumika katika maeneo hayo na zinasababisha uharibifu wa matumbawe.

Hata hivyo, aliwataka wavuvi hao kutumia nyavu zenye ukubwa wa nchi mbili ambazo ndizo zina uwezo wa kupitisha samaki wadogo na kutojihusisha na uvuvi wa madema ya waya ambayo yanachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa viumbe hai vya baharini.

Katibu wa Kamati ya Uvuvi Shehia ya Kiwengwa, Bakili Khamisi Alawi, alisema kamati ya uvuvi ya shehia hiyo itaendelea kupambana na uvuvi haramu kwa kuzingatia sheria na taratibu za serikali zinavyoelekeza ili kulinda rasilimali za bahari kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B, alilazimika kufika katika eneo hilo kwa lengo la kusuluhisha mgogoro kati ya wavuvi kutoka Kijiji cha Matemwe ambao wanatumia nyavu za macho madogo na kuvua samaki katika pwani ya Kijiji cha Kiwengwa kinyume cha utaratibu wa kamati ya uvuvi ya shehia hiyo na kusabaisha mgogoro mara kwa mara.

# Balozi Iddi awapa mtihani watakaochaguliwa Oktoba

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema viongozi wanaochaguliwa katika majimbo na wadi wana wajibu wa kuhakikisha kero zinazowakabili wananchi katika maeneo yao zinapatiwa ufumbuzi unaostahiki.

Alisema wajibu huo unakuwa dhima kwao kwa vile viongozi hao hutafakari, kujipima na hatimaye uwezo walionao nao huwashawishi kufikia hatua ya kuamua kutekeleza jukumu hilo la kuwatumikia wananchi.

Balozi Iddi alisema hayo jana wakati akiufungua mradi wa majisafi na salama uliotekelezwa kwa nguvu za wananchi wa Kijiji cha Fujoni Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja utakaokuwa na uwezo wa kuhudumia zaidi ya wananchi 300.

Alisema fedha za mifuko ya maendeleo ya majimbo zinatotolewa na serikali zote mbili Tanzania kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi Zanzibar ni msaada unaoongeza nguvu katika miradi iliyoanzishwa na wananchi.

Balozi Iddi ambaye ni Mwakilishi anayemaliza muda wake Jimbo la Mahonda, alisema zinapojitokeza changamoto kwenye miradi ya kijamii si vyema viongozi na wananchi wakajenga fikra za kuzisubiri taasisi husika.

Alieleza kwamba itapendeza iwapo wananchi na viongozi husika wakaongeza jitihada kwa kutafuta mbinu za kupata ufumbuzi wa changamoto hizo.

Balozi Iddi aliwaomba wananchi katika majimbo yao kuwa tayari kuwapokea wabunge, wawakilishi na madiwani wapya watakaopewa jukumu la kuwatumikia wakati utakapowadia baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "B", Rajab Ali Rajab, alisema viongozi wa majimbo kwa kushirikiana na wananchi wamekuwa wakiwekeza katika miradi ya kijamii hasa ile ya huduma za maji na afya kutokana na changamoto zinazoikumba jamii katika maeneo yao.

Hata hivyo, aliwashauri wananchi na kamati za maendeleo za majimbo, wadi na shehia kuzishirikisha taasisi zinazohusika na miradi wanayoianzisha ili kuepuka mapema matatizo yanayoweza kukwamisha maendeleo ya miradi hiyo.

Mkuu huyo wa Wilaya ya Kaskazini "B" alimpongeza Balozi Iddi anayemaliza muda wake wa uwakilishi katika Jimbo la Mahonda kwa kufanikiwa vyema utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi katika kipindi chake cha miaka mitano.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa Kaskazini Unguja, Iddi Ali Ame, aliwatahadharisha viongozi wanaopewa jukumu la kuwahudumia wananchi waepuke sababu zisizo na msingi zinazoweza kupelekea kuwavunja moyo wananchi wanaowasimamia.

Alisema mwananchi wakati wote wa harakati zake za kimaisha anahitaji kupata huduma za lazima na za msingi na pale inapotokea tatizo ndani ya miradi inayoanzishwa lazima ushirikiano wa pamoja upewe nafasi ya kipekee.

Mwenyekiti huyo wa CCM Mkoa wa Kaskazini Unguja alionya kwamba mbunge, mwakilishi au diwani yeyote atakayeshindwa kusimamia jukumu lake alilokabidhiwa chama hakitasita kumwajibisha hata kabla ya kumalizika kwa kipindi chake cha utumishi wa miaka mitano.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (kulia), akipokea zawadi ya madafu ya kitamli kutoka kwa wananchi wa Kijiji cha Fujoni, baada ya kuufungua mradi wa majisafi na salama wa kijijini hapo Wilaya ya Kaskazini "B", jana. **PICHA: OMPR – ZNZ**

# Sababu bajeti ya elimu kupaa zaanikwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amesema Serikali ya Zanzibar imeiongezea bajeti Wizara ya Elimu ili kuhakikisha wananchi wote wanapata elimu kama walivyoanzisha waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa semina ya maandalizi ya kujiunga na vyuo vikuu iliotayarishwa na Jumuiya ya 'Afrika Moja Movement' katika ukumbi wa Kariakoo Mjini Unguja, alisema serikali kupitia Wizara ya Elimu inaendelea kuifanyia kazi falsafa za waasisi ili kuhakikisha Zanzibar inazalisha wataalamu wanaoendana na soko la ajira.

Alisema ipo haja kwa wanafunzi kupatiwa taaluma juu ya kujiunga na elimu ya juu na namna ya kupata mikopo ili kuepusha usumbufu kwa wanafunzi na kuepuka kujiunga na vyuo visivyo sahihi kwao.

Said aliwaomba wanafunzi watakaopata nafasi ya masomo nje ya nchi kuwa wazalendo kwa kurejea nyumbani baada ya kuhitimu masomo na kusimamia mila, tamaduni na silka za nchi yao kwa kipindi chote wanapokuwa masomoni.

Aidha, aliwataka wanafunzi hao kusoma kwa bidii ili kulinda heshima ya Taifa na kupata maendeleo.

Aliwataka wanafunzi kutumia haki yao ya kikatiba kwa kwenda kupiga kura wakati utakapofika na kuhakikisha wanadumisha amani ya nchi yao pamoja na kuwataka kuepukana na vurugu zinazoashiria uvunjifu wa amani.

Naye Mratibu Mkuu wa Africa Moja Movement Unguja, Eshe Mtumwa Said, alieleza kuwa jumuiya yao inaendesha programu za kuwajengea uwezo vijana wa Kiafrika na kuwaunganisha vijana wa Afrika katika nyanja za kiuchumi, kiutamaduni na kiitikadi.

Alisema kuwa wanatoa programu za kuwasaidia vijana katika makundi mbali mbali wakiwamo yatima, wazee na hata watu wenye ulemavu.

Pia alisema changamato kubwa ambayo inawakumba wanafunzi wa sekondari na hata wale wa elimu ya juu ni kushindwa kujua fani wanazotaka kusoma, hali inayopelekea kuchagua fani zisizokuwa na soko.

Aliwasihi wanafunzi kusikiliza kwa makini maelezo watakayopatiwa ili kufanya maamuzi mazuri katika uchaguzi wa fani ambazo watakwenda kusoma vyuoni.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**GENERATE MONEY AND JOBS**
- Learn Designing winning Project Proposals
- Access Donors.
- Establish NGO
- **0784 505108/0718 437371/ 0769 5050108**


## *NIPASHE NI JIBU LAKO*

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**AMINA ATHUMAN JUMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3136/0006** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2019 katika shule ya Sekondari Sinde. Yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **OB/RB/6150/2020**

115869902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALEX R. NTANGULIGWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina **NISSAN EXTRAIL** yenye namba za usajili **T774 CGS** Chassis no. **SXU10-0034215,** Engine no. **5S129883.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**OB/RB/10732/2017**

115870002

## KUPOTEA OFFA YA KIWANJA

**MELKIOR PETER** MKAZI WA **BUSHUSHU** MANISPAA YA **SHINYANGA.**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFFA YA KIWANJA **NAMBA 79 KITALU "RR" MEDIUM DENSITY** BUSHUSHU KATIKA MANISPAA YA SHINYANGA.

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA MELKIOR PETER KWA SIMU **NAMBA 075482977**

**RB NAMBA SHY/RB/2020, CONTROL NAMBA 9910818192341.**

JACOB F. MWINUKA
AFISA ARDHI
MANISPAA SHINYANGA

AFISA ARDHI WA MANISPAA SHINYANGA

115870502

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ

**SIMON GIDION MWAKILEMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaj yenye namba za usajili **MC536 BLA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya polisi
**MBE/MBE/RB/602474/2020**

115870202

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**Abiud P Shoo** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba **MC. 858 AXS** aina ya **SANLG** yenye Chassis namba **LBRSPJB52F9029647** yenye engine namba **15949469.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake
Taarifa ya Polisi:
**NML/RB/363/2020.**

215869002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JOSEPH LAWRENCE MKANYIA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye Namba za Usajili **T.379 CYV.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu naye.
TAARIFA YA POLISI NI KUMB NI
**MBE/MBE/RB/606586/2020**

215870402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**

**MAKAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU WILAYA YA GEITA**

**SHAURI LA MADAI NA:36/2020**

**MDAI: ELIZABETH MALONGO**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: YOHANA SELEMANI WA NYAWILIMILWA (W) GEITA**

**AMRI:-**
Unaamriwa na mahakama uhudhurie hapa mahakamani mnamo tarehe 25-08 2020 saa 2:30 asubuhi bila kukosa usipo hudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo, na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama leo J TATU tarehe 17 mwezi 08-2020.

PRIMARY COURT MAGISTRATE
HAKIMU

115869102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;232/2020**

**Ombi la OCTAVIANA GERALD MKUDE,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu BEDA KOMBA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/08/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/08/2020.

115870702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;238/2020**

**Ombi la IDDY JUMA MUHERUKA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MOSHI MTANI KABULA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 26/08/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 20/08/2020.

115870802

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Lisekese**

**Usimamizi wa Mirathi 35/2020.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 31/7/2020 kabla huyo mwombaji hujateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani wawezi kukaguliwa. Tarehe 24/7/2020.

Sahihi ya Hakimu

115869302

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GIVEN ONIA NGAJILO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajil **T 469 DPY.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilcho karibu.
Taarifa ya polisi
**MBE/MBE/RB/614709/2020**

115870302

**IN THE RESIDENT MAGISTRATES COURT OF BUKOBA AT BUKOBA**

**CIVIL CASE NO. 10 OF 2015**

**1. NICKSON NELSON SAMSON @ NDYAMUKAMA......PLAINTIFF**
**2. JONSTON JOAS..........................................PLAINTIFF**
**3. AGNES GODFREY........................................PLAINTIFF**
**4. SIMON GERVASE........................................PLAINTIFF**
**5. ODILO OSWARD.........................................PLAINTIFF**
**6. JESCA DOMICIAN.......................................PLAINTIFF**
**7. NEEMA JOHN..............................................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**CHINA HENAN INTERNATIONAL COOPERATION GROUP (CHICO)...............1st DEFENDANT**
**CHICO-CRSG JOINT VENTURE.................2nd DEFENDANT**

**NOTICE OF MENTION**

**TO: CHICO-CRSG JOINT VENTURE C/O ANETH LWIZA ADVOCATE, WESTLAKE ATTORNEYS, BUKOBA. 0787425159**
**TAKE NOTICE** that the mentioned case has been set down for Mention on the 2nd day of SEPTEMBER, 2020 at 8:30 O'clock in the forenoon, Before Hon. W. YONA-RM your presence is therefore required on the date and the time indicated.
Given under my hand and the seal of the court this 21st day of AUGUST, 2020.

RESIDENT MAGISTRATE
BUKOBA

115869602


***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Maandamano mweusi apigwa risasi

**WASHINGTON,** Marekani

MAANDAMANO yamezuka katika Jimbo la Wisconsin nchini Marekani, baada ya polisi kumpiga risasi mtu mweusi.

Mwanamume huyo aliyetambuliwa kwa jina Jacob Blake, yuko mahututi hospitalini.

Video zilizotumwa kwenye mitandao ya kijamii zilionesha Blake akipigwa risasi kwa nyuma, wakati anajaribu kuingia kwenye gari katika mji wa Kenosha.

Mamlaka katika mji wa Kenosha imetangaza kuanza kutekelezwa kwa dharura, hali ya kutotoka nje usiku baada ya kuzuka kwa maandamano kutokana na upigaji risasi huo.

Mamia ya watu wameandamana hadi makao makuu ya polisi. Magari yalichomwa moto huku waandamanaji wakiwa wanapiga makelele wakisema: "Hatuwezi kurudi nyuma".

**Tunachopinga ni utumiaji wa nguvu kupita kiasi na pia namna mambo yanavyokuzwa haraka ikiwa ni suala la polisi na mtu mweusi huko Wisconsin.**

Katika tahadhari iliyotolewa kwa umma, polisi ilisema wanaofanya biashara saa 24 wasifunge kwa sababu ya wizi wa kimabavu na matukio ya ufyatuaji wa risasi.

Maofisa wa polisi walitumia mabomu ya machozi kutawanya mamia ya waandamanaji waliokiuka hatua ya kusalia ya nje. Gavana wa Wisconsin, Tony Evers, alishutumu tukio hilo la ufyatuaji risasi dhidi ya Blake ambaye inasemekana hakuwa na silaha.

"Wakati hatuna taarifa kwa sasa, tunachojua ni kwamba huyo siyo mtu wa kwanza kupigwa risasi au kujeruhiwa au kuuawa kiholela mikononi mwa maofisa katika jimbo letu au nchini mwetu," alisema katika taarifa Gavana Evers na kuongeza:

"Tunachopinga ni utumiaji wa nguvu kupita kiasi na pia namna mambo yanavyokuzwa haraka ikiwa ni suala la polisi na mtu mweusi huko Wisconsin," alisema Evers

Jina la Jacob Blake limesambaa kwenye mitandao ya kijamii, huku maelfu ya watu wakiwa wametia saini wakitaka maofisa waliohusika na tukio hilo la ufyatuaji wa risasi wakamatwe na kufunguliwa mashtaka.

Idara ya haki ya Wisconsin inayochunguza tukio hilo imeeleza kuwa maofisa waliohusika wameagizwa kwenda likizo ili uchunguzi ufanywe.

Katika video iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii, maofisa watatu walionekana wakionesha silaha zao kwa mwanaume anayesemekana kuwa ni Blake wakati anatembea kwenye eneo la kuegesha gari.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa alipofungua mlango na kuegemea kwenye gari, ofisa mmoja alionekana akimshika shati lake na kufyatua risasi.

Kisha, risasi saba zilisikika kwenye video hiyo, huku walioshuhudia tukio hilo wakisikika kupiga mayowe na kelele.

Hata hivyo, ofisa aliyehusika na tukio hilo bado hajatambuliwa rasmi.

Wakili maarufu wa haki za raia, Ben Crump alieleza kuwa familia ya Blake ilikuwa imewasiliana naye kutafuta usaidizi. **BBC**

# Mataifa 10 hayajapata ugonjwa wa corona

**LONDON,** Uingereza

UGONJWA wa virusi vya corona umesababisha vifo vya mamilioni ya watu katika mataifa mengi duniani.

Tangu kuzuka kwa ugonjwa huo Machi, mwaka huu mataifa mengi yameathiriwa kiuchumi baada ya kufungwa kwa mipaka.

Mataifa ya ulaya mengi yameathiriwa kiuchumi kutokana na kuzuka kwa ugonjwa huo ambao unadaiwa chimbuko lake lilianzia katika mji wa Wuhan uliopo katika Jimbo la Hubei.

Hata hivyo, licha ya ugonjwa huo kuathiri nchi nyingi duniani lakini kuna mataifa 10 ambayo hadi hivi sasa hayajakumbwa na ugonjwa huo, hawajawahi kuripoti kisa chochote cha mgonjwa wala kifo kilichotokana na ugonjwa huo, wananchi wake wamekuwa wakiendelea na mihangaiko kama kawaida.

Nchi hizo ni Palau, Micronesia, Marshall Islands, Nauru, Kiribati, Solomon Islands,Tuvalu, Samoa, Vanuatu, pamoja na Tonga

Nchi ya Palau taifa dogo linalozungukwa na bahari ya Pacific limejipatia watalii wengi. Mwaka 2019, watalii 90,000 walitembelea Palau, ikiwa ni idadi mara tano ya jumla ya idadi iliopo.

Mwaka 2017, takwimu za IMF zilionesha kwamba utalii ulichangia asilimia 40 ya kipato cha nchi hiyo cha kila mwaka. Lakini hilo ni kabla ya mlipuko wa virusi vya corona kuanza.

Ni miongoni mwa mataifa 10 duniani ambayo hayakuthibitisha mgonjwa yeyote wa corona. **BBC**




Rais wa Marekani, Donald Trump, akizungumza na wafuasi wake katika mji wa Yuma Jimbo la Arizona. **PICHA: AP**

# Ripoti: Ndege ya Ukraine ilipigwa kombora

**TEHRAN,** Iran

RIPOTI ya matokeo ya utafiti wa chombo kinachorekodi safari za ndege "Black Box" cha ndege ya abiria ya Ukraine, iliyotunguliwa Tehran Januari 08, 2020, imeonyesha ndege ilipigwa na makombora mawili katika muda wa sekunde 25.

Ripoti hiyo iliyotolewa Jumapili na Iran inaonyesha abiria walikuwa bado hai kwa muda baada ya athari za mlipuko wa kwanza kutokea. Tangazo hilo limetolewa na Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Iran, Touraj Dehghani-Zanganeh, ni hatua ya kwanza ya ripoti rasmi inayoeleza maudhui yaliyopatikana ya sauti za marubani na rikodi za takwimu, ambazo zilitumwa Ufaransa kusomwa Julai.

Tehran ilieleza kuwa iliitungua ndege ya Ukraine kwa bahati mbaya Januari, wakati wa mvutano wa hali ya juu baina yake na Marekani. Abiria wote 176 waliuawa.

Dehghani-Zanganeh alinukuliwa na Televisheni ya Taifa akisema: "Sekunde 19 baada ya kombora la kwanza kupiga ndege hiyo, sauti za marubani ndani ya ndege, zinaonyesha kwamba abiria walikuwa bado hai ... sekunde 25 baadae kombora la pili lilipiga ndege hiyo"

Iran imekuwa katika mazungumzo na Ukraine, Canada na nchi nyingine ambazo walikuwa na raia wao katika ndege hiyo iliyotunguliwa, na ambao wameshinikiza kuwapo uchunguzi wa kina juu ya ajali hiyo.

Jeshi la Kulinda Mapinduzi ya Iran, Revolutionary Guards walitungua ndege hiyo ya Ukraine iliyokuwa kwenye safari ya kimataifa, kwa kombora la kutoka ardhini kwenda angani Januari 8, baada ya ndege kuondoka Tehran.

Jambo ambalo baadae Tehran ilikubali kuwa ni kosa la kusikitisha lililofanywa na vikosi ambavyo vilikuwa katika hali ya juu ya tahadhari wakati wa mgogoro wake na Marekani.

Maofisa wa Iran na Ukraine wamekuwa wakifanya mazungumzo juu ya utaratibu wa fidia kwa familia za abiria waliouawa.

Duru nyingine ya mazungumzo hayo imepangwa kufanyika ifikapo Oktoba, mwaka huu. **VOA**

# Wanajeshi Mali kuongoza kipindi cha mpito

**BAMAKO,** Mali

JUMUIYA ya Kiuchumi ya nchi za Magharibi mwa Afrika, (ECOWAS), pamoja na kundi la wanajeshi waliofanya mapinduzi nchini Mali, wamekubaliana kufunga ukurasa wa enzi za rais aliyepinduliwa madarakani, Ibrahim Boubakar Keita.

Hata hivyo, mazungumzo yanatarajia kuendelea kuhusu serikali ya mpito kwa kipindi cha miaka mitatu kama ilivyopendekezwa Agosti 24 na kundi hilo la wanajeshi.

Kulingana na vyanzo vya ndani kutoka kundi hilo la wanajeshi walio madarakani na ECOWAS, Kundi la wanajeshi wanaoshikilia madaraka nchini Mali tangu walipompindua madarakani Rais Keita, Agosti 18, wanataka kuundwa kwa serikali ya mpito, ambayo itaongozwa na mwanajeshi watakaoongoza nchi kwa kipindi cha miaka mitatu.

Taarifa hiyo ilitolewa baada ya saa 48 ya mazungumzo kati ya ECOWAS, kupitia ujumbe wake uliokwenda mjini Bamako mwishoni mwa wiki iliyopita, na maofisa wa Baraza la Kitaifa la linaloshikilia madaraka nchini Mali. **RFI**

# COUTINHO BADO HAJUI ATACHEZA WAPI 2020-21



**LISBON,** Ureno

PHILIPPE Coutinho hajui majaliwa yake yatakuwa wapi wakati akiwa anarudi Barcelona kutoka Bayern Munich.

Coutinho amemaliza kipindi chake cha kucheza kwa mkopo Bayern kwa kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya ushindi wa 1-0 dhidi ya Paris Saint-Germain kwenye fainali Jumapili.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil anatarajiwa kuondoka moja kwa moja Barcelona kipindi hiki cha mwisho wa msimu, na kiungo huyo wa zamani wa Liverpool amehusishwa na mpango wa kurudi Ligi Kuu ya England.

Coutinho, ambaye alitokea benchi kwenye mchezo dhidi ya PSG, alisema anatarajia kuwa na msimu imara 2020-21 - lakini hajui wapi atakapokuwa.

"Sikuwahi kufikiria kuhusu hili. Natakiwa kurudi na nataka kufanya kazi kwa bidii na kuwa na mwaka mzuri," alisema akiiambia Movistar+. "Sijui kama nitakuwa Barcelona."

Huku Barca ikiwa imemaliza msimu wa 2019-20 bila taji lolote, Coutinho ameshinda mataji matatu kule Bayern, na pia alifunga wakati miamba hao wa LaLiga wakifumuliwa 8-2 kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Coutinho alifunga mabao mawili kwenye mchezo huo ambao pia alitokea benchi.

# Pogba atasaini Man United mkataba mpya-Raiola

**MANCHESTER,** England

PAUL Pogba atabaki Manchester United na kumekuwa na mazungumzo kwa ajili ya kusaini mkataba mpya, kwa mujibu wa wakala wake, Mino Raiola.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 27, ambaye alijiunga tena na timu hiyo akitokea Juventus kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 89, ana mwaka mmoja umebaki kwenye mkataba wake pale Old Trafford, ingawa United wanakipengele cha kumuongezea miezi 12.

Pogba mara kwa mara amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka klabuni hapo, huku kurudi Juve au kwenda Real Madrid ndiko ambako kunatajwa zaidi.

Hata hivyo, tangu apone majeraha ya kifundo cha mguu yaliyomuweka benchi muda mwingi wa msimu wa 2019-20, Pogba amethibitisha kuwa sehemu ya mipango ya Ole Gunnar Solskjaer na alikuwa sehemu ya kuwasaidia 'Mashetani Wekundu' hao kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Huku mlipuko wa virusi vya corona ukiwa umeleta athari kubwa ya kifedha hata kwa klabu kubwa, ni wazi kwamba hakutakuwa na ofa kubwa kwa ajili ya Pogba na mshindi huyo wa Kombe la Dunia sasa anajiandaa kusaini mkataba wa muda mrefu hapo United.

Akizungumza na Sky Sport Italia, Raiola alisema: "Bado yupo katikati ya mradi muhimu wa kiufundi. Hata katika miaka ya hivi karibuni, United haijataka mazungumzo ya wazi.

"Tunazungumza taratibu kuhusu kusaini mkataba mpya. Hakuna kinachosumbua kwa sasa."





# *Wakala aondoa hofu kwa Ibrahimovic*

**MILAN,** Italia

MINO Raiola hamtarajii Zlatan Ibrahimovic kuripoti kwenye mazoezi na AC Milan wiki hii, lakini ana "matumaini" straika huyo atabaki na Rossoneri hao.

Nahodha huyo wa zamani wa Sweden alijiunga na Milan kwa mkataba mfupi kutoka klabu ya Ligi Kuu ya Marekani (MLS), LA Galaxy Januari na amefunga mabao 10 katika mechi 18 za Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Ibrahimovic atakuwa mchezaji huru mwishoni mwa mwezi huu, lakini mazungumzo yanaendelea ili kumbakiza hapo kwenye dimba la San Siro.

Milan jana Jumatatu waliripoti kwenye mazoezi, lakini Raiola ambaye ni wakala wa Ibrahimovic alisema, bado hawajafikia muafaka na mteja wake na hivyo hawezi kuanza mazoezi.

Hata hivyo, bado Raiola ana matumaini kwamba nyota huyo mwenye umri wa miaka 38, ataiongoza Milan kwa msimu wa 2020-21.

Aliiambia Sky Sport Italia: "Sidhani kama atakuwapo kwenye mazoezi Jumatatu (jana). Tunazungumza, lakini hatujafikia makubaliano bado.

"Naamini si tatizo la kifedha, lakini mambo yatakaa sawa tu, kwani hata ndoa huwezi kufunga bila baadhi ya mambo kukamilishwa."

# Flick na utani wa Alcantara Bayern

**LISBON,** Ureno

HANSI Flick alitania kwamba, Thiago Alcantara amemwambia atabaki hapo Bayern Munich baada ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Thiago aliisaidia Bayern kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Paris Saint-Germain kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumapili na kulitwaa taji hilo kwa mara ya sita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2021, lakini anatarajiwa kuondoka klabuni hapo, huku akihusishwa na mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Liverpool pamoja na mabingwa wa FA, Arsenal.

Kocha wa Bayern, Flick alitania kwamba kiungo huyo anaweza kubaki, lakini alisema alitaka kumshukuru Thiago.

"Hapana, (Thiago) ameniambia mimi atabaki. Hapana, natania tu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Hapana, nilitaka tu kumshukuru yeye kwa kazi aliyoifanya. Kama nilivyowashukuru wachezaji wote.

"Sijui, hajui bado kwa sababu wote akili yetu ilikuwa kwenye fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya.

"Sasa tunahitaji kuona nini kitatokea katika siku chache zinazokuja."

Thiago ameshinda mataji saba ya Bundesliga, Ligi ya Mabingwa Ulaya moja na mataji mengi kadhaa tangu alipojiunga na Bayern akitokea Barcelona mwaka 2013.





# NEYMAR AIPONGEZA BAYERN AKIMWAGA CHOZI

**LISBON,** Ureno

NEYMAR amesema "kupoteza ni sehemu ya mchezo" wakati nyota huyo wa Paris Saint-Germain akimwaga machozi na kuwapongeza Bayern Munich kwa kulitwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

PSG walishindwa kutwaa taji lao la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya katika fainali yao ya kwanza, baada ya kukubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Bayern jijini Lisbon, Ureno juzi, Jumapili. Neymar alionyesha simanzi kubwa baada ya mchezo huo kwa PSG kushindwa kulibeba taji hilo wakiwa tayari wameshatwaa mataji yote ya Ufaransa kwa msimu wa 2019-20.

Baadaye Neymar aliandika kupitia ukurasa wake wa Twitter: "Kupoteza ni sehemu ya mchezo, tulijaribu kila kitu, tulipigana hadi mwisho.

"Shukrani kwa sapoti yetu na mapenzi mliyotuonyesha kutoka kwa kila mmoja. Hongereni Bayer."

Bao la kichwa la kipindi cha pili kutoka kwa Kingsley Coman lilitosha kuwafanya mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Bayern kulibeba taji hilo kwa mara ya sita.

Pia ilishuhudia Bayern wakitwaa mataji matatu kwa msimu wa nane mfululizo, huku PSG wakiwa wanamaliza msimu huu kama mabingwa wa Ligue 1, Coupe de France, Coupe de la Ligue na Trophee de Champions.

# Silva athibitisha kuondoka PSG

**LISBON,** Ureno

THIAGO Silva anayewaniwa na Chelsea amethibitisha kwamba ameichezea mechi yake ya mwisho Paris Saint-Germain baada ya kufungwa na Bayern Munich kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa juzi.

PSG walishindwa kutwaa taji lao la kwanza la Ligi ya Mabingwa baada ya kufungwa na Bayern ambao ni mabingwa wa Bundesliga na DFB-Pokal, kwa bao 1-0 jijini Lisbon juzi Jumapili na kumaliza msimu wakiwa na mataji matatu.

Silva alisaini kuongeza mkataba wa kubaki PSG hadi mwishoni mwa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati akiwa anahusishwa kuwaniwa na Chelsea na miamba ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Fiorentina.

Chelsea imeripotiwa kuwa na nafasi kubwa zaidi ya kumsajili nyota huyo wa PSG, Silva kwa uhamisho huru na mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 35, alielezea majaliwa yake baada ya mchezo huo.

"Huu ulikuwa ni mchezo wangu wa mwisho kwa Paris. Nina huzuni," alisema mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil akiambia RMC Sport.

Silva amefurahia mafanikio tangu amejiunga na PSG kutoka AC Milan kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 42 mwaka 2012.Nahodha huyo wa PSG ameshinda mataji saba ya Ligue 1, matano ya Coupe de France, sita ya Coupe de la Ligue na matano ya Trophee des Champions.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LEWANDOWSKI KINARA WA MABAO MICHUANO UEFA

## Asema kamwe usiache kuota, usikate tamaa wakati ukishindwa, kiduchu afikie rekodi ya...

**LISBON,** Ureno

ROBERT Lewandowski amesema "kamwe usiache kuota" baada ya nyota huyo wa Bayern Munich hatimaye kushinda taji lake la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya huku akiibuka mfungaji bora wa michuano hiyo.

**Bayern ilitwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya sita na kumaliza msimu wa 2019-20 ikiwa ni mataji matatu, bada ya juzi Jumapili kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Paris Saint-Germain kwenye fainali.**

Bao la kichwa la kipindi cha pili la Kingsley Coman ndilo lililotenganisha timu hizo mbili mjini Lisbon, ambapo Bayern iliweka historia ya kuwa timu ya kwanza kushinda mechi 11 mfululizo za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ulikuwa usiku wa kukumbukwa zaidi kwa Lewandowski, ambaye hakushinda Kombe la Ligi ya Mabingwa hapo kabla wakati akielekea kwenye fainali hiyo dhidi ya PSG.

Kwani katika msimu wa 2012-13, akiwa na Borussia Dortmund walifungwa kwenye fainali ya mashindano hayo na Bayern.

Lewandowski ambaye ameshinda taji la Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, mara nane amefurahia msimu huu kwa kufunga jumla ya mabao 55 katika mashindano yote.

Na amelezea mafanikio hayo kwa kuandika kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram: "Kamwe usiache kuota. Usikate tamaa wakati ukishindwa.

"Fanya kazi kwa bidii na utafanikisha malengo yako. Asanteni kwa sapoti yenu, kwa kuamini uwezo wetu. Sisi ni mabingwa wa Ulaya!"

Wakati Lewandowski hakufunga kwenye mchezo huo dhidi ya PSG, straika huyo wa Bayern ndiye aliyeibuka mfungaji bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2019-20.

Lewandowski alifunga mabao 15 kwa Bayern, matano zaidi ya yale ya nyota wa Dortmund, Erling Haaland na mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland alibakisha mabao mawili tu kuifikia rekodi ya Cristiano Ronaldo ya kufunga mabao mengi ya michuano hiyo kwa msimu mmoja.

## ZISIKUPITE

### GABRIEL, ARSENAL WAMALIZANA

MLINZI wa kati wa Lille na Brazil, Gabriel Magalhaes mwenye umri wa miaka 22, amekubali kujiunga na Arsenal na atakamilisha uhamisho wa pauni milioni 27 wiki ijayo. ***(The Guardian)***

### FIGO: MESSI USIENDE MADRID

LUIS Figo hatarajii mshambuliaji na nahodha wa Barcelona, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, raia wa Argentina kufuata nyayo zake kwa kuondoka Barcelona kwenda Real Madrid. ***(Marca)***

### KOEMAN KWA MARTINEZ, GARCIA

KOCHA mpya wa Barcelona, Ronald Koeman anataka kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 23 raia wa Argentina, mlinzi wa kati wa Manchester City, Mhispania Eric Garcia,19, na mlinzi wa pembeni wa Valencia na Hispania, Jose Gaya, 25. ***(Sport)***

### VILLA WAJITOSA KWA EDOUARD

ASTON Villa itatoa ofa ya pauni milioni 30 kwa straika wa Celtic na Ufaransa, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 22. ***(The Scottish Sun)***

### KLOPP ATAJWA BARCA

MGOMBEA wa nafasi ya urais wa klabu ya Barcelona, Jordi Farre amesema amefanya mazungumzo na kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp. ***(Sport)***

### COUTINHO KUBAKI BARCELONA

RONALD Koeman angependa kiungo wa kimataifa wa Brazil, Philippe Coutinho kuwa sehemu ya mipango yake - baada ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, kumaliza kipindi chake cha kucheza kwa mkopo kule Bayern Munich msimu huu. ***(Mundo Deportivo)***

### YAMTAKA GIANNOULIS

NEWCASTLE imetoa ofa ya pauni milioni 4.5 ili kumsajili mlinzi wa kushoto wa Klabu ya PAOK ya nchini Ugiriki, Dimitris Giannoulis mwenye umri wa miaka 24. ***(Manu Lonjon via Sports Lens)***

### ARTETA ATAJA MSAIDIZI WAKE

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anamtaka kocha wa Brentford, Andreas Georgson kama mmoja wa wasaidizi wake katika kikosi chake. ***(London Standard)***

### IBRAHIMOVIC HAJASAINI MILAN

MSHAMBULIAJI Zlatan Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 38, bado hajasaini mkataba mpya na AC Milan. Mkongwe huyo atakuwa mchezaji huru mwishoni mwa mwezi huu. ***(Gazzetta dello Sport)***

### CR7 KAMPELEKA FERNANDES UTD

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Cristiano Ronaldo 'CR7' "alimpendekeza" kiungo wa Ureno, Bruno Fernandes mwenye umri wa miaka 25, kwa Manchester United, amesema mlinzi wa zamani wa United, Patrice Evra. ***(The Guardian)***

### HANSEN ATHIBITISHA UNITED

STRAIKA wa klabu ya Tromso ya nchini Norway, Isak Hansen-Aaroen mwenye umri wa miaka 16, amethibitisha uhamisho wake wa kwenda Manchester United kupitia mtandao wa kijamii. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

## Yanga yaitibulia JKT kwa Yondani

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Klabu ya JKT Tanzania umesema tetesi za uongozi wa Yanga kuhitaji kumrejesha beki wao, Kelvin Yondani zimewakwamisha kupata saini ya nyota huyo kwa ajili ya kuboresha kikosi cha timu yao kuelekea msimu wa 2020/21.

Yanga ilitangaza kuachana na Yondani baada ya kushindwana katika mazungumzo ya kusaini mkataba mpya, jambo lililoivutia JKT Tanzania kuanza mchakato wa kuipata huduma yake, lakini hivi karibuni klabu yake hiyo ya zamani imekuwa ikihusishwa na kutaka kumrejesha tena.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Makamu Mwenyekiti wa JKT Tanzania, Thabiti Baraji, alisema walikuwa wakimhitaji Yondani na wamekuwa wakimtumia nyota wao, Mwinyi Kazimoto kwa ajili ya kuzungumza naye ila kwa sasa inaonekana kushindikana.

"Tulimtumia Kazimoto kuongea na Yondani na baadaye tukutane naye viongozi, lakini imeshindikana kupata huduma yake baada ya kupata taarifa kwamba Yanga wanahitaji kumrejesha nyota huyo katika kikosi chao," alisema Baraji.

Alisema mbali na Yondani pia wameshindwa kupata huduma ya mshambuliaji wa Mtibwa Sugar, Jaffer Kabaya kwa sababu ya kushindwa kulipa dau la Sh. milioni 28 ambazo alikuwa akihitaji ili kusaini mkataba na klabu hiyo.

## Dodoma Jiji yaanika majembe ya 2020/21

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji iliyopanda daraja na kutarajia kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, imetangaza majina ya wachezaji 26 itakaowatumia kwenye msimu wa mpya wa 2020/21.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ramadhani Juma 'Raju', jana alitangaza wachezaji watakaounda kikosi chao kuwa ni makipa: Hussein Masalanga, Emmanuel Mseja na Aron Kalambo aliyesajiliwa kutoka Prisons akitoka kucheza kwa mkopo KMC.

Kwa upande wa mabeki aliwataja kuwa ni Anderson Solomon, Aboubakar Ngalema, Ibrahim Ngecha, Mbwana Kibacha, Hassan Kapona, George Wawa aliyesajiliwa kutoka Singida United, Jukumu Kibanda aliyesajiliwa akitokea Namungo FC, Augustino Ngata na Justine Omari.

Viungo walitajwa kuwa ni Rajab Seif, Jamal Mtegeta, Omari Kanyoro, Deus Kigawa, Salmin Hoza aliyepelekwa kwa mkopo kutoka Azam FC, Cleophace Mkandala aliyesajiliwa kutoka Prisons, Pter Mapunda aliyesajiliwa kutoka Mbeya City, na Dickson Ambundo kutoka Gor Mahia ya Kenya.

Washambuliaji aliwataja kuwa ni Anuary Jabir, Khamis Mcha kutoka Lipuli, Santon Thomas, Seif Karihe ambaye ni straika wa zamani wa Azam na Ruvu Shooting, na Mnaigeria Miachael Chinedu kutoka Alliance FC.

# SENZO AANZA NA JUKUMU MFUMO WA LALIGA YANGA

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Yanga umesema kuelekea mabadiliko ya kimfumo yanayoendelea ndani ya klabu hiyo, utafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na Mtendaji Mkuu wa zamani wa Klabu ya Simba, Senzo Mazingisa, kwa kuwa ana uzoefu mkubwa na masuala ya soka.

Senzo aliamua kujiuzulu Simba Agosti 9, mwaka huu na kisha kusaini mkataba wa kufanya kazi na Yanga, kwa kile alichoeleza kuwa amekosa furaha ndani ya 'Wekundu wa Msimbazi' hao ikiwa ni pamoja na kupishana kimtazamo.

**Akizungumza na waandishi wa habari, jana Makao Makuu ya Yanga, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Dk. Mshindo Msolla, alisema kwa sasa wanaamini wapo na mtu sahihi katika masuala ya ushauri katika klabu hiyo.**

"Bado tupo kwenye mabadiliko na tayari tumeshaanza kwa kushirikiana na watu wa La Liga, kikubwa ambacho tunakifanya ni kuwa na watu sahihi ambao watatupeleka kwenye mafanikio.

"Tayari tumeanza kufanya kazi na Senzo, ambaye ana uwezo mkubwa kwenye masuala ya michezo, katika vikao vyetu vya La Liga ameanza kutoa mchango wake hivyo tunaamini tumepata mtu sahihi," alisema Msolla.

Kwa upande wa Senzo alisema, malengo yake ni kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na viongozi wa Yanga wakiongozwa na mwenyekiti pamoja na viongozi wengine wote kwa kuwa anafahamu majukumu yake ya kazi.

"Mwenyekiti anafahamu majukumu yangu ya kazi, kikubwa ni kusimama katika ukweli na uwazi ili kufikia malengo ambayo tumejiwekea," alisema Senzo, ambaye kwa kipindi kifundi ndani ya Simba, alijenga kukubalika na mashabiki wa klabu hiyo.

**UNAKOSAJE?**




Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM, wadhamini wa Klabu ya Yanga, Mhandisi Hersi Said, akiwa na msanii wa Bongo Fleva, Rajab Abdul Kahali 'Harmonize' (kushoto) ambaye atatumbuiza kwenye kilele cha Wiki ya Mwananchi Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: YANGA**

# *Hitimana atoa sababu kipigo Namungo kwa Azam FC*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Hitimana Thierry, amesema kipigo cha mabao 2-1 walichokipata dhidi ya Azam FC juzi katika Uwanja wa Chamazi jijini Dar es Salaam, kilitokana na wao kutokuwa na muda mrefu wa mazoezi, huku wapinzani wao wakijifua kwa mwezi mzima sasa.

Akizungumza baada ya mechi hiyo maalumu kwa ajili ya Tamasha la Azam Festival, kocha huyo alisema haoni tatizo lolote kwa timu yake kupoteza mechi hiyo.

"Sijui kama inapaswa kufurahi au kuhuzunika, lakini ilikuwa mechi nzuri, ila sisi hatukuwa na muda mrefu wa mazoezi wakati wenzetu wana mwezi mzima sasa wakiwa mazoezini," alisema akitoa tathmini ya mechi hiyo.

Namungo itaiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika na ilikuwa ina baadhi ya wachezaji wapya ambao licha ya kuwa nao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, pia wataonekana kwenye michuano hiyo ya kimataifa.

Mchezo huo pia ulikuwa kipimo kizuri kwa Namungo ambayo inatarajia kushuka Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha Jumapili wiki hii kumenyana na Simba kwenye mechi ya Ngao ya Jamii ambayo ni maalum kwa ajili kuukaribisha msimu mpya wa Ligi Kuu 2020/21.

Katika mechi hiyo ya juzi, ambayo pia Azam iliitumia kwa ajili ya kuwatambulisha wachezaji wake wa msimu wa 2020/21, mabao yake yaliwekwa kambani na Mzambia Obrey Chirwa dakika ya 33 na Andrew Simchimba dakika ya 66.

Bao pekee la Namungo lilifungwa dakika ya 62, kupitia mchezaji mpya waliyemsajili akitokea Singida United, Mghana Steven Sey.

Tamasha hilo pia lilinogeshwa kwa burudani ya muziki kutoka kwa Ally Kiba.

# Michezo

Jumanne Agosti 25, 2020

Nipashe




Lewandowski kinara wa mabao michuano UEFA UKURASA 22




Wachezaji wa Bayern Munich wakishangilia kwa kutwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Paris Saint-Germain kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Luz jijini Lisbon, Ureno juzi. Bao pekee lilifungwa na Kingsley Coman dakika ya 59. **HABARI UK. 21**

# Yanga yamaliza na Carlinhos, Yacouba

## ●●● Kufunga mtaa leo wakimpokea kiungo huyo fundi kutoka Angola, Harmonize ndani Jumapili...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kocha Mkuu mpya wa Yanga, Mrundi Cedric Kaze sasa akitarajiwa kutua nchini Ijumaa, klabu hiyo imeweka wazi kuwa kiungo kutoka Angola, Carlos Fernandes 'Carlinhos' na straika raia wa Burkina Faso, Sogne Yacouba, ndio watakaofunga dirisha la usajili kwa upande wa timu hiyo.

**Kiungo Carlinhos anayejiunga na Yanga akitokea G.D. Interclube ya Angola, yeye atatua leo wakati Yacouba ambaye ni mshambuliaji akitokea Klabu ya Asante Kotoko ya Ghana, akitarajiwa kutua keshokutwa, Alhamisi.**

Akizungumzia usjio wa wachezaji hao ambao watakamilisha usajili wa timu hiyo kuelekea msimu mpya wa 2020/21, Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM, ambao ni wadhamini wa Klabu ya Yanga, Mhandisi Hersi Said, aliwataka Wanayanga kujitokeza kwa wingi leo kumpokea kiungo huyo atakapotua leo.

"Tumebakiza usajili wa wachezaji wawili ambao mmoja atatua leo, tutamtambulisha atakapotua, Wanayanga wajitokeze kwa wingi leo kumpokea," alisema Hersi huku akisita kumtaja jina, lakini tayari Nipashe lilishaelezwa kuwa ni Carlinhos.

Kuhusu kocha mkuu, Hersi alisema ataanza safari Alhamisi akitokea Canada na kuwasili nchini Ijumaa, tayari kuanza kuinoa timu hiyo ambayo msimu huu imefanya usajili mkubwa zaidi pengine katika historia ya klabu hiyo.

"Tayari amekamilisha taratibu zote na Alhamisi ataanza safari ya kuja nchini kuanza kuinoa timu yetu," alisema Hersi ambaye amesimamia usajili wote wa Yanga msimu huu.

Kuhusu Yacouba, Ofisa Habari wa Yanga, juzi alisema kuwa kinachomchelewesha straika huyo kutua nchini ni kutokana na anga la kwao bado kuwa limefungwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, lakini sasa wanamatarajio ya kumpokea Alhamisi.

"Yeye anatarajiwa kutua Alhamisi kwani viwanja vya ndege vya kwao vilitarajiwa kufunguliwa Agosti 25 (leo), hivyo hadi Alhamisi atakuwa amewasili," alisema.

Wachezaji wengine wa kigeni wapya waliosajiliwa Yanga msimu huu ni pamoja, mshambuliaji Mghana Michael Sarpong ambaye sasa atawania namba na Yacouba pamoja na washambuliaji wazawa, Ditram Nchimbi na Waziri Junior.

Katika nafasi ya kiungo wapya waliosajiliwa mbali na Carlinhos ni viungo wawili kutoka Klabu ya AS Vita ya DR Congo, Mukoko Tonombe na Tuisila Kisinda, hivyo kuifanya Yanga hadi sasa kusajili jumla ya nyota wapya watano.

Katika hatua nyingine, kwenye kilele cha Wiki ya Mwananchi Jumapili wiki hii, kitakachofanyika Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam, Yanga imepania kuwakuna mashabiki wake vilivyo kwa burudani kutoka kwa wasanii mbalimbali wakiongozwa na msanii nguli wa Bongo Fleva, Rajab Abdul Kahali 'Harmonize'.

# Sven: Simba hii ni bandika bandua

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, amesema viwango vilivyoonyeshwa na wachezaji wapya katika kikosi hicho vinampa matumaini ya kuwa na kikosi kipana kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu na michuano ya kimataifa.

Sven alitoa kauli hiyo baada ya kushuhudia nyota hao wapya wakicheza kwa kuelewana katika mechi ya kilele cha Wiki ya Simba maarufu Simba Day, walipoivaa Vital'O ya Burundi.

"Safu ya ushambuliaji ipo vizuri, nina uhakika wa kumpanga mtu, endapo kutakuwa na mgonjwa au kutumikia adhabu basi sitapata wakati mgumu wa kuumiza kichwa," alisema Sven na kuongeza.

"Kutakuwa na ushindani mkubwa wa namba, jambo ambalo litasababisha kuumiza kichwa kufikiri nimwanzishe nani, hii ndiyo maana ya kikosi kipana kwa timu mchezaji anayetoka na anayeingia kuwa na uwezo mkubwa," alisema.

Katika mechi ya juzi, kikosi kilichoanza dhidi ya Vital'O kilishinda 2-0 hadi dakika 45 za kipindi cha kwanza, na baada ya mapumziko Sven alibadili kikosi kizima, ambapo kilichoingia kilicheka na nyavu mara nne na kuifanya Simba kushinda 6-0.

Katika safu ya ulinzi iliyoanza, ilikuwa chini ya mabeki wa kati wapya mzawa Ibrahim Ame na Mkenya Joash Onyango ambao walionyesha kuelewana vizuri, huku kiungo mchezaji mpya, Mzambia Larry Bwalya akifanya makubwa wakati mshambuliaji aliyesajiliwa akitokea KMC, Charles Ilamfya na Mkongomani aliyetokea Lusaka Dynamos, Chris Mugalu kila mmoja akicheka na nyavu mara moja, hali inayoonyesha itaongeza ushindani wa namba dhidi ya John Bocco na Meddie Kagere.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042